# Kiswahili

## Kitabu cha Mwanafunzi

2



Tusome Early Literacy Programme

## Yaliyomo


Utangulizi ........ ii
Dibaji ........ ii
Wiki ya 1 ........ 1
Wiki ya 2 ........ 6
Wiki ya 3 ........ 11
Wiki ya 4 ........ 16
Wiki ya 5 ........ 21
Wiki ya 6 ........ 26
Wiki ya 7 ........ 31
Wiki ya 8 ........ 36
Wiki ya 9 ........ 41
Wiki ya 10 ........ 46
Wiki ya 11 ........ 51
Wiki ya 12 ........ 56
Wiki ya 13 ........ 61
Wiki ya 14 ........ 66
Wiki ya 15 ........ 71
Wiki ya 16 ........ 76
Wiki ya 17 ........ 81
Wiki ya 18 ........ 86
Wiki ya 19 ........ 91
Wiki ya 20 ........ 96
Wiki ya 21 ........ 101
Wiki ya 22 ........ 106
Wiki ya 23 ........ 111
Wiki ya 24 ........ 116
Wiki ya 25 ........ 121
Wiki ya 26 ........ 126
Wiki ya 27 ........ 131
Wiki ya 28 ........ 136
Wiki ya 29 ........ 141
Wiki ya 30 ........ 146

## Utangulizi

Tangu kupata uhuru, serikali ya Kenya imetambua elimu kama mojawapo ya haki za kimsingi za binadamu; kwa hivyo imejitolea kuwapa wananchi wake wote elimu bora. Raslimali nyingi zimewekezwa ili kuimarisha upatikanaji, umuhimu, usawa na ubora, vipengee ambavyo vimeboresha miundomsingi na kuongeza idadi ya wanaohudhuria masomo katika nyanja tofauti za elimu na mafundisho.

Serikali inatambua ya kwamba ili kuweza kushindana katika nyanja za kimataifa na kuimarika kiuchumi, taifa linahitaji elimu inayowawezesha wananchi kuwa wabunifu, kupata elimu ya kudumu maishani na wanaoweza kufanya kazi zilizo tata na zenye changamoto. Elimu pia inafaa kuwawezesha wananchi kutatua shida katika jamii, kukata shauri, kufanya kazi bila kufuatiliwa, kuwajibika na pia waweze kusoma, kupiga mambomsasa na kupata ujuzi wa kujidhihirisha. Maendeleo ya kudumu yanahitaji kila binadamu apate maarifa ya karne ya 21, ujuzi, mtazamo na maadili yanayohitajika kudumisha maisha ya siku za usoni. Mkazo unatiliwa kwenye elimu inayowezesha kusoma na kufanya hesabu. Nchi ya Kenya imefanya maendeleo katika kuhakikisha ubora wa elimu. Miradi mbalimbali imewekwa ili kuangazia ubora wa elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi.

Kitabu hiki cha Tusome, bila shaka, kitaimarisha masomo kuanzia darasa la 1 na la 2 ya shule za msingi kwenye somo la kujua kusoma na kuandika. Mpangilio wa masomo unahakikisha ya kwamba wanafunzi wote nchini Kenya wanaweza kusoma na kuelewa ifikapo mwisho wa mwaka. Kwa hivyo, nawahimiza washirika wetu waendelee kusaidia sekta ya elimu katika utekelezaji wa mikakati na mbinu ili kuboresha elimu.

**Prof. Jacob T. Kaimenyi**, PhD, FICD, EBS

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

## Dibaji

Lengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote bila kuzingatia hali yao ya kuichumi na kijamii. Mabadiliko yamefanywa ili kuimarisha sekta ya elimu. Mabadiliko haya yana mtazamo wa kuifanya nchi ishindane kimataifa. Mipango ya utafiti kama vile Tathmini ya Kitaifa na Ufuatiliaji wa Mafanikio ya Masomo (NASMLA) na Muungano wa Kusini na Mashariki mwa Afrika wa Kufuatilia Ubora wa Elimu (SACMEQ) inaonyesha kuwa kuna umuhimu wa kuboresha mafanikio katika uwezo wa kusoma na kufanya hesabu.

Maendeleo yaliyofanyika hivi karibuni katika nchi ya Kenya yalionyesha kuwa kuna haja zaidi ya kuwa na mfumo wenye kina wa kuhakikisha ubora wa elimu. Mabadiliko haya yamo katika Katiba ya Kenya (2010) na Ruwaza ya Kenya ya 2030. Katiba ya Kenya inahakikishia kila mtoto nchini masomo ya msingi yasiyo na malipo. Vilevile, Ruwaza ya Kenya ya 2030 inatarajia kuhakikisha kuwa kuna mabadiliko ya kimaendeleo nchini na pia ushindani katika nyanja za kimataifa ifikapo mwaka wa 2030. Kati ya matarajio ni kutoa elimu bora na mafundisho ili kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi wa hali ya juu. Mfumo uwe wa kupatia wanafunzi ujuzi wa kazi utakaounganisha nchi na soko la kimataifa. Nakala ya Kikao Cha Bunge Nambari 14 ya 2012 inaonyesha njia mwafaka na wanafunzi asilimia mia moja waweze kukamilisha masomo katika elimu ya msingi bila kuathiri ubora wa elimu.

Wizara ya elimu inatazamia kuboresha elimu katika madarasa ya chini ya shule za msingi hasa ikizingatia uwezo wa kusoma na kuandika na kufanya hesabu. Mradi wa Kitaifa wa Tusome unaodhaminiwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Amerika (USAID) na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID), unakusudia kuboresha matokeo ya kuweza kusoma na kuandika katika madarasa ya 1 na ya 2. Mradi huu unalenga kuboresha uwezo wa walimu wa kuelekeza darasani, kuhakikisha wanafunzi wamepata vitabu sahihi vya kusoma na vya ziada, na kuwaelekeza walimu kupitia kwa wakufunzi wa mashauri ya walimu (TAC Tutors) na walimu wakuu. Halikadhalika, utaanzisha njia mwafaka za kufuatilia na kutathmini matokeo ambayo itaunganisha mafunzo na matokeo katika kujifunza kusoma na kuandika. Mradi huu utatumia teknolojia ili kuimarisha mafunzo ya kujua kusoma na kuandika na kuongeza uwezo wa sekta ya elimu kuboresha matokeo ya masomo.

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu, ninawasihi washikadau wote kushirikiana ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa Tusome umefua dafu.

**Dkt. Belio R. Kipsang**

Katibu Mkuu,

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia: Idara ya Elimu

Tamka sauti.

■ **M m** **A a** **U u**

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

● **ma** **maa** **mu** **muu**

Soma silabi na maneno.

bi na mu
**binamu**

sha nga zi
**shangazi**

m jo mba
**mjomba**

a ta m pa
**atampa**

Tamka sauti.

▲ **K k** **T t** **L l**

Soma sehemu za neno na neno lote.

hu m tembelea
**humtembelea**


a ka wa peleka
**akawapeleka**

a ka m kumbuka
**akamkumbuka**

a ka mwambia
**akamwambia**

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi | Umoja | | Wingi |
|---|---|---|---|---|---|
| **m**jomba | — | **wa**jomba | **m**jukuu | — | **wa**jukuu |
| **m**zazi | — | **wa**zazi | **m**zee | — | **wa**zee |



## Okitoi

Okitoi, babu na nyanya wanaishi katika kijiji cha Makutano. Dada yake Pendo anaishi na baba na mama katika jiji la Kisumu. Shule zikifungwa, Okitoi humtembelea shangazi yao Amina. Shangazi humsalimia, "Hujambo Okitoi karibu nyumbani." Naye humjibu, "Sijambo shangazi asante sana." Akiwa kwa shangazi, yeye hucheza na binamu zake, Karimu na Sila.

Siku moja, Pendo na binamu zake walienda kwa mjomba. Wakamwamkua mjomba, "Shikamoo mjomba." Mjomba alijibu kwa furaha, "Marahaba wanangu." Mjomba akawapeleka kwenye mbuga ya wanyama. Mara Pendo akamkumbuka kaka yake Okitoi akasema, "Okitoi angefurahia sana kuwaona wanyama hawa."

Mjomba akamwambia Pendo atampa picha ya wanyama ili ampelekee Okitoi. Pendo akatabasamu na kusema, "Asante mjomba."

Tamka sauti.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ■ | **N n** | **O o** | **W w** |

Tamka sauti ya herufi na usome silabi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ● | **no** | **wo** | **to** | **noo** |

Soma silabi na maneno.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ▬ | ma ra fi ki | wa za zi | m sa a da | m ku bwa |
| | **marafiki** | **wazazi** | **msaada** | **mkubwa** |

Tamka sauti.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ▲ | **E e** | **H h** | **I i** |

Tamka sauti ya herufi na silabi.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ⬬ | **he** | **hi** | **hee** | **hii** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ★ | ku ni letea | tu sherehekee |
| | **kuniletea** | **tusherehekee** |
| | ni ta wa elezea | na wa heshimu |
| | **nitawaelezea** | **nawaheshimu** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| | | |
|---|---|---|
| ◆ | **Sentensi** | **Kinyume** |
| | Mti huu ni **mkubwa** | - Mti huu ni **mdogo**. |
| | Huu ndio **mwanzo** wa hadithi | - Huu ndio **mwisho** wa hadithi. |
| | Talia ni **rafiki** yangu | - Talia ni **adui** yangu. |
| | Chai hii ni **tamu** | - Chai hii ni **chungu**. |



## Jamaa yangu

Hodi hodi marafiki, shairi nawaletea,
La baba na mama yangu, wazazi walonilea,
Majina ya jamaa yangu, wote nitawaelezea,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Kaka, dada umenipa, ndugu zangu wa pekee,
Na marafiki umenipa, tucheze tusherehekee,
Binamu ni watoto, wa mjomba na shangazi,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Shangazi, amu na mjomba, ndugu za baba na mama,
Si lazima kuwaomba, msaada wanatumana,
Baba mdogo, mkubwa, Mungu ametuletea,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Wa mwisho na wa muhimu, waliozaa wazazi wangu,
Wananipenda nawaheshimu, babu na bibi yangu,
Hadithi zilizo tamu, michezo hucheza yangu,
**Asante Mola wangu, baraka kuniletea.**

Tamka sauti.

■ Ss Bb Yy

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ja ma a - jamaa**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ba | nga | ja | mba | a | Zi |
| sha | ma | bu | m | bi | jo |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Yule ni **m**jukuu wangu | — | Wale ni **wa**jukuu wetu. |
| **M**jomba amefika | — | **Wa**jomba wamefika. |
| **M**zazi ameenda kazini | — | **Wa**zazi wameenda kazini. |
| **M**ke wangu anapika | — | **Wa**ke wetu wanapika. |

## Nyati na sungura



Tamka sauti.

■ **Z z** **D d** **G g**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● **da** **zi** **gu** **ga**

Soma silabi na maneno.

▬ si mu ru nu nu vi fa a ta ra ki li shi

**simu** **rununu** **vifaa** **tarakilishi**

Tamka sauti.

▲ **J j** **R r** **F f**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

⬬ **je** **ro** **fo** **jo**

Soma sehemu za neno na neno lote.


★ ku wasiliana
**kuwasiliana**
zi me rahisisha
**zimerahisisha**

wa li tumia
**walitumia**
zi na weza
**zinaweza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Simu **hii** ni **yangu** | - | Simu **hizi** ni **zetu.** |
| Kompyuta **hii** ni **yangu** | - | Kompyuta **hizi** ni **zetu.** |
| Printa **hii** ni **yangu** | - | Printa **hizi** ni **zetu.** |
| Tarakilishi **hii** ni **yangu** | - | Tarakilishi **hizi** ni **zetu.** |



## Vifaa vya ofisini

Ofisi huwa na vifaa vya kufanyia kazi mbalimbali. Vifaa hivi hufanya kazi kuwa rahisi. Watu hutumia tarakilishi kutuma barua pepe. Hapo awali watu walitumia simu za waya pekee kuwasiliana. Sasa tuna simu za rununu pia ambazo zinaweza kutumika mahali popote. Njia za kisasa za kutuma ujumbe zimerahisisha mawasiliano.

Tamka sauti.

■ **v** **sh** **dh**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● **vo** **sha** **dhi** **dhu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

▬

ku zu ngu m za
**kuzungumza**

ma wa si li a no
**mawasiliano**

ku si ki za
**kusikiza**

ku ta za ma
**kutazama**

ru ni nga
**runinga**

a ra fa
**arafa**

Tamka sauti.

▲ **ny** **ch** **ng'**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● **nye** **cho** **cha** **ng'u**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

ku amini
**kuamini**

wa na wasiliana
**wanawasiliana**

wa na weza
**wanaweza**

tu na weza
**tunaweza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

Simu ya rununu iko **juu ya** meza.
Simu huwekwa **mbali na** maji.
Aliongea kwa simu **chini ya** mti.
Nyaya za simu huwekwa **juu ya** mti.



## Teknolojia

Katika dunia ya leo, watu wengi wanawasiliana kwa kutumia simu za rununu. Simu ya rununu ni simu ya mkononi. Simu za rununu hutumika kwa kuzungumza, kutuma na kupokea ujumbe mfupi au arafa. Pia hutumiwa kutuma barua pepe. La ajabu ni kuwa siku hizi tunaweza kutuma pesa, kusikiza redio na hata kutazama runinga kwenye simu zetu. Pia kuna michezo tele katika simu za rununu. Siku hizi hata watoto wadogo wanaweza kutumia simu hizi. Ni vigumu kuamini kuwa kuna wakati simu za rununu hazikuwepo.

Tamka sauti.

■ th gh ng

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.

Kwa mfano: **si mu - simu**.

★

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ya | ta | a | hu | fa | ki | mu | li | fa |
| shi | wa | ru | ba | si | no | ra | nu | vi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● 

| Umoja -angu | | Wingi -etu |
|---|---|---|
| Hii ni simu **yangu** | - | Hizi ni simu **zetu.** |
| Hii ni tarakilishi **yangu** | - | Hizi ni tarakilishi **zetu.** |
| Hii ni ofisi **yangu** | - | Hizi ni ofisi **zetu.** |
| Hii ni runinga **yangu** | - | Hizi ni runinga **zetu.** |

## Teknolojia



Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i | e | u | e |
| chi | che | pu | pe |
| **mchi** | **mche** | **mpu** | **mpe** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m chi | m pu nga | m re fu |
| **mchi** | **mpunga** | **mrefu** |
| m ge ni | s ti ma | s ta re he |
| **mgeni** | **stima** | **starehe** |

Tamka silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| e | e | i | a |
| re | ge | ti | ta |
| **mre** | **mge** | **sti** | **sta** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a ki twanga | a ka mwona | a ki wasili |
| **akitwanga** | **akamwona** | **akiwasili** |
| a li washa | a li nawa | ku m karibisha |
| **aliwasha** | **alinawa** | **kumkaribisha** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

Mchi umo **ndani ya** kinu.

Alilala **nyuma ya** nyumba.

Mgeni aliketi **juu ya** kiti.

Aliwasha taa na kuiweka **kando ya** birika.



## Mgeni nyumbani

Rehema alikuwa akitwanga mpunga kwenye kinu kwa mchi mrefu. Akamwona mgeni akiwasili langoni. Rehema akamsalimia na kumkaribisha kwenye chumba cha wageni. Aliwasha taa na kufungua televisheni ili mgeni astarehe. Rehema aliwasha moto haraka haraka na kupika wali na nyama ya kukaanga. Aliandaa chakula na kumkaribisha mgeni mezani. Mgeni alinawa na kupakua chakula baada ya maombi. Rehema na mgeni wakala wali kwa nyama.

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **a** | **a** | **o** |
| **zi** | **za** | **da** | **do** |
| **nzi** | **nza** | **nda** | **ndo** |

Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| ku si n zi a | b la n ke ti |
| **kusinzia** | **blanketi** |
| a li a nza | fo ro nya |
| **alianza** | **foronya** |

Soma silabi.


| | | | |
|---|---|---|---|
| **e** | **i** | **e** | **i** |
| **ke** | **ki** | **se** | **si** |
| **mke** | **mki** | **mse** | **msi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| a li amua | a li imba | a li sinzia |
| **aliamua** | **aliimba** | **alisinzia** |
| a li nawa | a li washa | a li m sikia |
| **alinawa** | **aliwasha** | **alimsikia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Neno** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| **ali**amua | — | **haku**amua |
| **ali**imba | — | **haku**imba |
| **ali**anza | — | **haku**anza |
| **ali**sinzia | — | **haku**sinzia |



## Kapendo

Jana jioni Kapendo aliamua kusikiliza redio. Redio ilikuwa ikicheza nyimbo tamutamu. Mara Kapendo alianza kusinzia. Mama yake akaja na kusema, "Kapendo, amka. Kumbuka kunawa miguu yako kabla ya kulala. Sitaki uchafue blanketi lako." Kapendo alijibu, "Ndio mama." Muda si muda, Kapendo alisinzia tena. Alianza kuota kuwa yuko kwenye kitanda chenye godoro zito na foronya nyororo. Kitanda hicho kilikuwa kinapaa angani. Alisikia sauti ikimwita. Hapo ndipo alimsikia mama yake akisema, "Mwanangu, amka. Nenda ukalale."

Tamka sauti.

■ ng' dh ny ng mb

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m chi - mchi**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ta | m | ki | do | mba | ra |
| mbo | wi | fo | nda | ti | ng'o |
| nya | ro | go | chi | pi | dha |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

●

| Umoja -angu | | Wingi -etu |
|---|---|---|
| Huu ni mchi **wangu** | - | Hii ni michi **yetu.** |
| Huu ni mlingoti **wangu** | - | Hii ni milingoti **yetu.** |
| Huu ni mpira **wangu** | - | Hii ni mipira **yetu.** |
| Huu ni mti **wangu** | - | Hii ni miti **yetu.** |

## Maina, kizee na ng'ombe



Tamka sauti.

■ dh sh

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● dha she dhi sho

Soma silabi na maneno.

▬ na dhi fu
**nadhifu**

dha ha bu
**dhahabu**

sa hi hi sha
**sahihisha**

m ko mbo zi
**mkombozi**

Tamka sauti.

▲ m k

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| o | i | a | a |
| ko | ki | wa | wa |
| mko | mki | mwa | twa |


Soma silabi na maneno.

★ a na itwa — **anaitwa**
hu wa tuza — **huwatuza**
a na penda — **anapenda**
wa ki soma — **wakisoma**

Sarufi: Soma maneno haya.

◆

| Umoja (ni) | | Wingi (tu) |
|---|---|---|
| **ni**natuzwa | - | **tu**natuzwa |
| **ni**naitwa | - | **tu**naitwa |
| **ni**napenda | - | **tu**napenda |
| **ni**nasoma | - | **tu**nasoma |




## Mwalimu wetu

Jina langu ni Kajuzi. Ninasoma katika Shule ya Mkombozi. Niko katika darasa la pili. Mwalimu wetu anaitwa Kazamoyo. Yeye huvalia nadhifu kila siku. Pia anapenda kuvaa saa ya dhahabu mkononi. Yeye hubeba kalamu mbili za wino. Moja ni ya kusahihishia madaftari yetu na nyingine ya kuandikia kazi zake. Mwalimu Kazamoyo hutufunza kusoma na kuandika kwa njia ya kipekee. Kila mara yeye hutumia chati za hisabati, herufi na picha za kufundishia maneno. Wanafunzi wakisoma vizuri yeye huwatuza kwa wimbo mtamu.

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **ia** | **ia** | **ia** | **ia** |
| **mia** | **dhia** | **tia** | **lia** |

Soma silabi na maneno.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ku bwa | re ji s ta | mi cho ro | ku hi fa dhi a |
| **kubwa** | **rejista** | **michoro** | **kuhifadhia** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **wa** | **wa** | **wa** | **wa** |
| **bwa** | **mbwa** | **kwa** | **mwa** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi me bandikwa | hu tumia |
| **zimebandikwa** | **hutumia** |
| zi me pambwa | ku onyesha |
| **zimepambwa** | **kuonyesha** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja (Hili)** | | **Wingi (Haya)** |
|---|---|---|
| **Hili** ni darasa langu | – | **Haya** ni **ma**darasa yetu. |
| **Hili** ni dawati langu | – | **Haya** ni **ma**dawati yetu. |
| **Hili** ni jina langu | – | **Haya** ni **ma**jina yetu. |
| **Hili** ni yai langu | – | **Haya** ni **ma**yai yetu. |




## Darasa la akina Hamisi

Darasa la akina Hamisi linavutia sana. Hamisi analipenda darasa lake. Yeye na rafiki yake Karani hutumia dawati moja. Kuta za darasa lao zimepambwa kwa chati zenye michoro mizuri. Picha za wanyama na mimea zimebandikwa kwenye kuta hizo. Kuna kabati kubwa la kuhifadhia vitabu vya mwalimu na wanafunzi. Juu ya kabati kuna sajala au rejista yenye majina ya wanafunzi wote. Karibu na kabati kuna kalenda ya kuonyesha siku na tarehe.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ka ya mba - kayamba**.

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ri | gi | ma | ya | a | ze |
| mbi | ngo | mba | ka | fi | ta |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| **Wakati** | **Kitenzi** |
|---|---|
| jana | **wali**tufunza |
| juzi | **wali**tufunza |
| leo | **wana**tufunza |
| kesho | **wata**tufunza |
| kesho kutwa | **wata**tufunza |

## Ala za muziki



Soma silabi.

| | | |
|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** |
| **wa** | **wa** | **wa** |
| **njwa** | **shwa** | **swa** |

Soma silabi na maneno.

mwa li mu
**mwalimu**
hu zu ni shwa
**huzunishwa**

m go njwa
**mgonjwa**
ke nge le
**kengele**

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **ea** | **ea** | **ua** | **ua** |
| **mea** | **lea** | **mua** | **lua** |


Soma sehemu za neno na neno lote.

a ka amua
**akaamua**
wa ka kusanyika
**wakakusanyika**

a li yo isoma
**aliyoisoma**
tu li furahia
**tulifurahia**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **mwa**limu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **mwa**nafunzi | - | Hawa ni **wa**nafunzi. |
| Huyu ni **m**kuu wa shule | - | Hawa ni **wa**kuu wa shule. |
| Huyu ni **m**gonjwa | - | Hawa ni **wa**gonjwa. |



## Darasani

Kengele ilipolia, sote tulitulia darasani kusubiri mwalimu. Mwalimu mkuu, Bi. Fahamu, alikuja na kutuarifu kuwa mwalimu wetu alikuwa mgonjwa. Tulihuzunishwa na habari hiyo. Kiranja wetu, Galana, akaamua kutusomea hadithi tamu. Hadithi aliyoisoma Galana ilituchekesha sana. Tulifurahia kusoma hadithi tamutamu. Kengele ya pili ilipolia, wanafunzi wote na walimu wakakusanyika mbele ya ofisi ya mwalimu mkuu.

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **i** | **o** |
| **ta** | **ta** | **ti** | **to** |
| **kta** | **sta** | **sti** | **sto** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma k ta ba | m li ngo ti | bu s ta ni |
| **maktaba** | **mlingoti** | **bustani** |
| m ku bwa | m si ngi | m kuu |
| **mkubwa** | **msingi** | **mkuu** |

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **i** | **i** | **u** | **e** |
| **li** | **si** | **ku** | **ke** |
| **mli** | **msi** | **mku** | **mke** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma kubwa | m refu | ku pendeza | ku leta |
| **makubwa** | **mrefu** | **kupendeza** | **kuleta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huu ni **m**lingoti **m**refu | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**refu. |
| Huu ni **m**lingoti **m**fupi | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**fupi. |
| Huu ni **m**lingoti **m**kubwa | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**kubwa. |
| Huu ni **m**lingoti **m**zuri | - | Hii ni **mi**lingoti **mi**zuri. |
| Huu ni **m**kebe **m**dogo | - | Hii ni **mi**kebe **mi**dogo. |



## Shule ya Msingi ya Tuigoin

Shule ya Msingi ya Tuigoin ni shule kubwa sana. Ina madarasa makubwa ya mawe. Madarasa yana madirisha makubwa ya kuleta mwangaza na hewa safi. Shule hii pia ina ofisi ya mwalimu mkuu, maktaba na chumba cha walimu. Nje ya ofisi kuna bustani ya maua ya kupendeza. Pia kuna mlingoti mrefu wa bendera. Shule hii ina uwanja mkubwa. Kando ya uwanja kuna vyoo safi vya wanafunzi na walimu.

Tamka sauti.

■ **ms** **sh** **aa**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **bu sta ni - bustani**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| sta | da | ni | ma | u | sa |
| na | ba | kta | wa | bu | ta |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Kuakifisha**

Mlingoti huu ni mrefu.
Mfupa huu ni mkubwa.
Mkebe huu ni mdogo.
Mchoro huu ni mbaya.

## Shule yangu



Tamka sauti.

■ **ny** **ng**

Tamka sauti ya herufi na silabi.

● **nye** **nya** **ngi** **ngo**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u koo | sha nga zi | m ku bwa |
| **ukoo** | **shangazi** | **mkubwa** |
| bi na mu | nya nya | za ngu |
| **binamu** | **nyanya** | **zangu** |

Soma silabi.

| | | |
|---|---|---|
| **o** | **o** | **u** |
| **do** | **jo** | **ku** |
| **mdo** | **mjo** | **mku** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

| | |
|---|---|
| a li ni eleza | a ka endelea |
| **alinieleza** | **akaendelea** |
| a ka ni eleza | ni ta mu ita |
| **akanieleza** | **nitamuita** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆ **Umoja –angu** **Wingi –etu**

**Huyu** ni nyanya **yangu** - **Hawa** ni nyanya **zetu**.
**Huyu** ni babu **yangu** - **Hawa** ni babu **zetu**.
**Huyu** ni shangazi **yangu** - **Hawa** ni shangazi **zetu**.
**Huyu** ni binamu **yangu** - **Hawa** ni binamu **zetu**.



## Ukoo wetu

Siku moja nyanya yangu alinieleza kuhusu ukoo wetu. Aliniambia kuwa yeye alikuwa na watoto watano. Nyanya akanieleza kuwa kaka za baba yangu nitawaita amu. Nyanya akaendelea kusema kuwa dada za baba yangu ni shangazi zangu. Nao watoto wao wote nitawaita binamu. Nyanya akanieleza kuwa kaka wa mama yangu ni mjomba. Dada mkubwa wa mama yangu nitamuita mama mkubwa.

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| e | i | o | u |
| ze | zi | zo | zu |
| mze | mzi | mzo | mzu |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a ja bu | ma do a do a | m zo ga |
| **ajabu** | **madoadoa** | **mzoga** |
| hu mu u a | bwa wa | ng'o mbe |
| **humuua** | **bwawa** | **ng'ombe** |

Soma silabi.


| | | | |
|---|---|---|---|
| o | i | o | e |
| to | ti | mo | me |
| mto | mti | mmo | mme |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa na po mwona | wa ka m shauri |
| **wanapomwona** | **wakamshauri** |
| wa li shangaa | ya li yo fanana |
| **walishangaa** | **yaliyofanana** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mama mmoja | **1** | — | mama watatu | **3** |
| dada mmoja | **1** | — | dada wawili | **2** |
| babu mmoja | **1** | — | babu wanne | **4** |
| shangazi mmoja | **1** | — | shangazi watano | **5** |



## Boma la Wakoli

Katika kijiji cha Serere paliishi Mzee Wakoli. Mzee huyu alikuwa na ng’ombe wengi sana. Siku moja, ng’ombe wao mmoja alizaa ndama wa ajabu. Ndama huyu alikuwa na madoadoa yaliyofanana na ya chui. Watu wa Serere wakamshauri Wakoli amuue yule ndama. Wakoli na jamaa yake wakakataa. Kesho yake wanakijiji wa Serere walishangaa kuona boma lote la Wakoli limetoweka. Mahali pake palikuwa na bwawa la maji. Tangu siku hiyo, watu wa Serere wanapomwona ngo’mbe wa madoadoa, hutaka kumuua mara moja na kutupa mzoga wake msituni. Lakini wao hushangaa na kuogopa wanapokumbuka kisa hiki.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno
Kwa mfano: **ba bu - babu**


★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ba | nya | bi | mba | sha | wa |
| zi | m | go | da | ma | mu |
| bwa | do | ku | nga | bu | jo |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **m**kulima | - | **wa**kulima |
| **m**zazi | - | **wa**zazi |
| **m**jomba | - | **wa**jomba |
| **m**tawa | - | **wa**tawa |
| **m**vuvi | - | **wa**vuvi |

## Mali shambani



# Sehemu za mwili

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku pu mu li a | ku si ki li zi a | ku o ne a |
| **kupumulia** | **kusikilizia** | **kuonea** |
| ku li a | ku nywe a | ma a lu mu |
| **kulia** | **kunywea** | **maalumu** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ma cho | m do mo | ki pa ji | vi si gi no |
| **macho** | **mdomo** | **kipaji** | **visigino** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu m peleka | ya me oshwa |
| **humpeleka** | **yameoshwa** |
| ku hakikisha | zi me katwa |
| **kuhakikisha** | **zimekatwa** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **–ako** | | **–angu** |
|---|---|---|
| macho **yako** | - | macho **yangu** |
| masikio **yako** | - | masikio **yangu** |
| mikono **yako** | - | mikono **yangu** |
| magoti **yako** | - | magoti **yangu** |



## Sehemu za mwili

Kila sehemu ya mwili wako ni muhimu. Pua hutumiwa kupumulia, masikio kusikilizia na macho kuonea. Mikono hufanya kazi mbalimbali. Mdomo nao hutumiwa kwa kulia na kunywea. Miguu humpeleka mtu kokote atakako kwenda. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa kila sehemu ya mwili wetu ni safi kuanzia utosini hadi wayoni.
Pia hakikisha kichwa, kipaji, macho, pua na masikio yameoshwa vizuri. Tumia jiwe maalum kusugua visigino na nyayo. Hakikisha kucha zako zimekatwa. Ukifanya hivyo, utakuwa na afya bora.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mwi li | m do mo | ki chwa |
| **mwili** | **mdomo** | **kichwa** |
| ki de vu | ma sha vu | shi ngo |
| **kidevu** | **mashavu** | **shingo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li kubaliana | ya ka ongezeka |
| **walikubaliana** | **yakaongezeka** |
| ya ka changia | hu wa shikilia |
| **yakachangia** | **huwashikilia** |

Sarufi. Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mtoto ana **m**guu mfupi | - | Watoto wana **mi**guu mifupi. |
| Mvulana ana **m**kono mrefu | - | Wavulana wana **mi**kono mirefu. |
| Mzee ana **m**fupa mgumu | - | Wazee wana **mi**fupa migumu. |
| Mzazi ana **m**gongo mpana | - | Wazazi wana **mi**gongo mipana. |



## Wanakijiji wa mwili

Wanakijiji wa Mwili walikutana kuzungumzia maisha yao. Mikono ikasema, “Sisi hufanya kazi zote za kusaidia mwili.” Miguu ikakatiza, “Nasi huubeba mwili mzima.” Macho yakachangia, “Sisi huhitajika kwa kuona.” Masikio yakaongezea, “Nasi huhitajika kusikia.” Mdomo ukasema, “Kwa nini mnadhani ni ninyi peke yenu mnaofanya kazi? Sote tuna kazi maalum. Shingo hukibeba kichwa. Vidole husaidia mikono. Kucha husaidia vidole. Shavu hurembesha uso. Kidevu hushikilia Mashavu na Mdomo.” Wote kijijini Mwili walikubaliana naye kuwa kila mmoja wao ni muhimu.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m do mo - mdomo**

★


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ma | si | a | do | o | gu |
| mo | cho | ki | pu | u | m |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| **Neno** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| shavu | - | **ma**shavu |
| sikio | - | **ma**sikio |
| goti | - | **ma**goti |
| bega | - | **ma**bega |

## Binti wa mfalme



Soma silabi na maneno.

m ku li ma — **mkulima**

ki fye ke o — **kifyekeo**

t re k ta — **trekta**

ma sha mba — **mashamba**

a li ng'o a — **aling'oa**

mbe gu — **mbegu**

ho da ri — **hodari**

sho ka — **shoka**

ma za o — **mazao**

ti nga ti nga — **tingatinga**

Soma sehemu za neno na neno lote.

zi li zo m patia — **zilizompatia**

a li po taka — **alipotaka**

a li ya uza — **aliyauza**

li li kuwa — **lilikuwa**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Shamba hili ni kubwa | - | **Ma**shamba haya ni **ma**kubwa. |
| Shamba hili ni dogo | - | **Ma**shamba haya ni **ma**dogo. |
| Jembe hili ni dogo | - | **Ma**jembe haya ni **ma**dogo. |
| Jembe hili ni kubwa | - | **Ma**jembe haya ni **ma**kubwa. |
| Tingatinga hili ni dogo | - | **Ma**tingatinga haya ni **ma**dogo. |
| Tingatinga hili ni kubwa | - | **Ma**tingatinga haya ni **ma**kubwa. |



## Mkulima hodari

Katika kijiji cha Nguvumali, kulikuwa na mkulima hodari sana. Aliitwa Mzee Bidii. Yeye alikuwa na mashamba makubwa na madogo. Alipotaka kukata nyasi katika shamba dogo alitumia kifyekeo, kisha akalima kwa jembe. Kama shamba lilikuwa kubwa, alitumia shoka kukatia miti mikubwa. Pia aling'oa mizizi ya miti kwa uma. Baadaye alitumia trekta au tingatinga kulima shamba hilo. Alipanda mbegu nzuri zilizompatia mazao mengi. Aliyauza mazao hayo na kuwa tajiri.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ki bi na f si | mi ho go | mi me a |
| **kibinafsi** | **mihogo** | **mimea** |
| ma tu mi zi | ma hi ndi | ma ja ni |
| **matumizi** | **mahindi** | **majani** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i na yo pandwa | u ku lima |
| **inayopandwa** | **ukulima** |
| wa ku lima | ki bi nafsi |
| **wakulima** | **kibinafsi** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari. |
| **M**zee huyu anatembea | - | **Wa**zee hawa wanatembea. |
| **M**tu huyu ni mgeni | - | **Wa**tu hawa ni wageni. |
| **M**tumishi huyu ni mcheshi | - | **Wa**tumishi hawa ni wacheshi. |



## Ukulima

Ukulima ni kazi muhimu sana kwa ufanisi wa nchi. Kuna aina mbili za wakulima. Baadhi ya wakulima hulima ili wapate mazao kwa matumizi yao ya kibinafsi. Wakulima wengine hulima ili wauze mazao na kupata fedha. Mimea inayopandwa kwa matumizi ya nyumbani ni kama vile: mahindi, mboga, mihogo, ndizi na viazi vitamu. Mimea inayopandwa kwa ajili ya kuuza ni kama vile: kahawa, maua, majani chai na miwa.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m be gu - mbegu**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mbe | pe | go | a | sho |
| je | ho | me | ndi | ma |
| mi | hi | gu | ra | ka |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **M**kulima huyu ni hodari | - | **Wa**kulima hawa ni hodari. |
| **M**toto huyu si mtukutu | - | **Wa**toto hawa si watukutu. |
| **M**zazi huyu ana bidii | - | **Wa**zazi hawa wana bidii. |
| **M**jukuu huyu anafanya kazi | - | **Wa**jukuu hawa wanafanya kazi. |

## Wema hauozi



Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| m chwa | gha la ni | vi gi ngi |
| **mchwa** | **ghalani** | **vigingi** |
| u ha ri bi fu | ki chu guu | m du du |
| **uharibifu** | **kichuguu** | **mdudu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu fananishwa | wa na m jua |
| **hufananishwa** | **wanamjua** |
| wa na o fanya | i ta wa letea |
| **wanaofanya** | **itawaletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mchwa ni **m**dudu **m**dogo | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**dogo. |
| Mchwa ni **m**dudu **m**haribifu | - | Mchwa ni **wa**dudu **wa**haribifu. |
| Mchwa ni **m**dudu mwenye bidii | - | Mchwa ni **wa**dudu wenye bidii. |
| Mchwa huyu ni **m**kali | - | Mchwa hawa ni **wa**kali. |



## Mchwa

Mchwa ni mdudu ambaye ana sifa nyingi. Watu wanamjua mchwa kwa uharibifu wake. Kwa mfano mchwa anaweza kuharibu mazao ghalani na kula miti na vigingi vya nyumba. Mbali na uharibifu, mchwa ana sifa nzuri kutokana na bidii yake. Je, wajua kwamba mchwa hujenga nyumba yake kwa mate? Nyumba hii huitwa kichuguu. Watu wanaofanya kazi kwa bidii hufananishwa na mchwa. Mara nyingi watu wanaofanya kazi kwa bidii hupata manufaa.

Soma silabi na maneno.

ko mba mwi ko
**kombamwiko**

ki wa vi
**kiwavi**

ku mbi ku mbi
**kumbikumbi**

n zi
**nzi**

ki ro bo to
**kiroboto**

vi nywa ji
**vinywaji**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa ka sameheana
**wakasameheana**

ku wa alika
**kuwaalika**

wa li hudhuria
**walihudhuria**

a me chafua
**amechafua**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Ki**pepeo **m**dogo **a**napepea | - | **Vi**pepeo **wa**dogo **wa**napepea. |
| **Ki**wavi **m**dogo **a**nakula | - | **Vi**wavi **wa**dogo **wa**nakula. |
| **Ki**roboto **m**dogo **a**meniuma | - | **Vi**roboto **wa**dogo **wa**meniuma. |
| **Ki**vunjajungu **m**dogo **a**naruka | - | **Vi**vunjajungu **wa**dogo **wa**naruka. |



## Sherehe ya wadudu

Katika shamba la Ngomeni kulizuka vita kali kati ya kombamwiko na kiwavi. Kombamwiko alikuwa amechafua vazi la kiwavi ambalo lilikuwa maridadi sana. Kiroboto aliona ni heri aandae sherehe na kuwaalika wadudu wote. Mwendo wa saa nne, wadudu walianza kuingia. Viwavi, siafu, nyuki, nzi, panzi na kumbikumbi walihudhuria. Wadudu wakala vyakula na kunywa vinywaji vitamu. Mwishowe wakasameheana. Tangu siku hiyo wadudu waliishi kwa umoja.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nyi gu - nyigu**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| bo | si | nyu | vi | gu | pe |
| chwa | chu | o | ngu | zi | nyi |
| ro | m | to | du | n | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mchwa **huyu** ni **m**dogo | - | Mchwa **hawa** ni **wa**dogo. |
| Mbu **huyu** ni **m**baya | - | Mbu **hawa** ni **wa**baya. |
| Nyigu **huyu** ni **m**kubwa | - | Nyigu **hawa** ni **wa**kubwa. |
| Nzi **huyu** ni **m**chafu | - | Nzi **hawa** ni **wa**chafu. |

## Wadudu



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ma wi ngu | ngu ru mo | ra di |
| **mawingu** | **ngurumo** | **radi** |
| mbi ngu | m cha che | mwa nga za |
| **mbingu** | **mchache** | **mwangaza** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu ki ruka ruka | ya ka tanda |
| **tukirukaruka** | **yakatanda** |
| i ka badilika | i li yo funikwa |
| **ikabadilika** | **iliyofunikwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| **Tuli**ona mwalimu | - | **Hatu**kuona mwalimu. |
| **Tuli**kuwa darasani | - | **Hatu**kuwa darasani. |
| **Tuli**chezea kwao | - | **Hatu**kuchezea kwao. |
| **Tuli**sikia sauti | - | **Hatu**kusikia sauti. |



## Anga

Hali ya anga ilikuwa tulivu. Tulikuwa uwanjani tukirukaruka na kucheza. Mara hali ya hewa ikabadilika. Mawingu meusi yakatanda angani. Mbingu ilionekana kama iliyofunikwa kwa blanketi jeusi. Muda mfupi baadaye, tukaona mwangaza mkali. Kisha tukasikia mingurumo ya radi. Kwa woga, sote tulitorokea darasani. Punde si punde, mvua nyingi ikaanza kunyesha. Maji yakajaa kila mahali. Mvua ilipopusa sote tulirudi uwanjani tukachezea maji ya mvua.

Soma silabi na maneno.

ma nu faa
**manufaa**

hu bu ru di sha
**huburudisha**

she re he ke a
**sherehekea**

ba fu ni
**bafuni**

ma go njwa
**magonjwa**

ku o ge le a
**kuogelea**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★

ku tapika
**kutapika**

ya ta chafuka
**yatachafuka**

hu ya tamani
**huyatamani**

hu tu letea
**hutuletea**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Sentensi** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| Pika viazi | - | **Usipike** viazi. |
| Cheza kandanda | - | **Usicheze** kandanda. |
| Elea juu ya maji | - | **Usielee** juu ya maji. |
| Chafua ukuta | - | **Usichafue** ukuta. |



## Maji

Maji ya manufaa, mvua hutuletea,
Yaweza leta balaa, usije sherehekea,
Siyaone yatapakaa, ukaanza kutegemea,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Bila maji hakika, viumbe tutasumbuka,
Chakula sitakipika, wala vyombo kusafishika,
Majumba yatachafuka, magonjwa ya kutapika,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Twapenda kuyachezea, njiani hata bafuni,
Kuogelea na kuelea, kama samaki majini,
Wanyama nayo mimea, maji huyatamani,
**Maji ndio uhai, maisha huburudisha.**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ku sa fi sha - kusafisha**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| pi | ku | o | sa | sha | ka |
| fu | ga | nywa | fi | a | ni |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● 

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **Mwa**nadamu **yu**ko wapi? | - | **Wa**nadamu **wa**ko wapi? |
| **M**nyama **yu**ko wapi? | - | **Wa**nyama **wa**ko wapi? |
| **M**dudu **yu**ko wapi? | - | **Wa**dudu **wa**ko wapi? |

## Maji



Soma silabi na maneno.


| | |
|---|---|
| te k no lo ji a | ru nu nu |
| **teknolojia** | **rununu** |
| ta ra ki li shi | vi tu li zo |
| **tarakilishi** | **vitulizo** |
| te le vi she ni | ru ni nga |
| **televisheni** | **runinga** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i me badilika | wa me itikia |
| **imebadilika** | **wameitikia** |
| zi me tapakaa | zi me enea |
| **zimetapakaa** | **zimeenea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Tarakilishi **hii** ni kubwa | - | Tarakilishi **hizi** ni kubwa. |
| Runinga **hii** ni nzuri | - | Runinga **hizi** ni nzuri. |
| Simu **hii** ni mpya | - | Simu **hizi** ni mpya. |
| Rununu **hii** ni nyeupe | - | Rununu **hizi** ni nyeupe. |



## Teknolojia

Dunia imebadilika, teknolojia imeingia,
Bara, pwani imefika, wote wameitikia,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Redio nazo tunazo, nyumbani na kwenye simu,
Mawaidha na vitulizo, mafundisho ya kuheshimu,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Tarakilishi twatumia, shuleni hata kazini,
Zina michezo ya kuvutia, zitumie kwa makini,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Runinga zimeenea, zaitwa televisheni,
Picha video kuonea, muziki pia sikizeni,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Simu zimetapakaa, kila pahali nchini,
Za rununu na za waya, twatuma hata matini,
**Teknolojia tunayo, dunia imebadilika.**

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| u hu nzi | u vu mi li vu | Ki bye go |
| **uhunzi** | **uvumilivu** | **Kibyego** |
| ku a ji ri | bi ri ka | m hu nzi |
| **kuajiri** | **birika** | **mhunzi** |
| su fu ri a | ka ra i | vyu ma |
| **sufuria** | **karai** | **vyuma** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu tengeneza | ku tengeneza |
| **hutengeneza** | **kutengeneza** |
| wa me tengeneza | i na hitaji |
| **wametengeneza** | **inahitaji** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Huyu ni **m**hunzi | - | Hawa ni **wa**hunzi. |
| Huyu ni **m**walimu | - | Hawa ni **wa**limu. |
| Huyu ni **m**susi | - | Hawa ni **wa**susi. |
| Huyu ni **m**bunge | - | Hawa ni **wa**bunge. |



## Mzee Kibyego

Watu wengi siku hizi hutegemea sana kazi za kuajiriwa. Ni vyema pia kutafuta kazi ambazo unaweza kujiajiri wewe mwenyewe.

Kwa njia hii watu wengi watatengeneza kazi na kuwaajiri wengine.

Kwa mfano, Mzee Kibyego hufanya kazi ya uhunzi. Yeye hutengeneza vitu kama karai, sufuria na birika za vyuma. Mzee Kibyego alifundishwa kazi hii na babake. Kwa kawaida, kazi hii inahitaji nguvu nyingi sana. Pia inahitaji uvumilivu. Mhunzi ni lazima atumie moto mkali na ujuzi mwingi sana. Kazi hii humletea mzee Kibyego manufaa makubwa.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ma ji - maji**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| a | ma | mu | ji | nywa |
| nga | ki | ru | si | ku |
| li | ni | vu | m | me |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo** | | **Wakati ujao** |
|---|---|---|
| Walimu **wana**cheka | - | Walimu **wata**cheka. |
| Wananchi **wana**msalimia | - | Wananchi **wata**msalimia. |
| Wanyama **wana**enda | - | Wanyama **wata**enda. |
| Wanafunzi **wana**pata | - | Wanafunzi **wata**pata. |

## Mwalimu ni malaika



# Haki za watoto

Soma silabi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **a** | **a** | **a** | **a** |
| **wa** | **wa** | **wa** | **wa** |
| **zwa** | **pwa** | **ndwa** | **swa** |

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| dhu lu ma | ku si ki zwa | ku fu ra hi a |
| **dhuluma** | **kusikizwa** | **kufurahia** |
| ku li pwa | ku li ndwa | a na pa swa |
| **kulipwa** | **kulindwa** | **anapaswa** |


Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ha wa ruhusiwi | i na m linda |
| **hawaruhusiwi** | **inamlinda** |
| a me fikisha | wa na paswa |
| **amefikisha** | **wanapaswa** |

Sarufi: Soma maneno haya.

**Maneno ya kuamuru na ukanusho**

| Neno | Kukanusha | Neno | Kukanusha |
|---|---|---|---|
| linda | **usi**linde | fanya | **usi**fanye |
| saidia | **usi**saidie | chapa | **usi**chape |



## Haki za watoto

Katiba ya Kenya inamlinda mtoto kutokana na dhuluma za kila aina. Kila mtoto ambaye amefikisha umri wa miaka sita anapaswa kuwa shuleni. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi ya kulipwa. Watoto wanapaswa kufanya kazi za kuwasaidia wazazi nyumbani. Ni hatia kwa mtu yeyote kumuadhibu mtoto kwa kumchapa. Watoto pia wana haki ya kulindwa, kupata matibabu yanayofaa na haki ya kusikizwa. Ni haki ya watoto kucheza na kufurahia maisha yao.

Soma silabi na maneno.

wa le ma vu
**walemavu**

ma gu ru du mu
**magurudumu**

wa si o o na
**wasioona**

ki ma u mbi le
**kimaumbile**

wa si o si ki a
**wasiosikia**

bi na da mu
**binadamu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na o zaliwa
**wanaozaliwa**


wa na hitaji
**wanahitaji**

ku wa saidia
**kuwasaidia**

hu chechemea
**huchechemea**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Mama **a**siyeona anakuja | - | Mama **wa**sioona wanakuja. |
| Nyanya **a**siyesikia analala | - | Nyanya **wa**siosikia wanalala. |
| Baba **a**siyetembea anacheka | - | Baba **wa**siotembea wanacheka. |
| Shangazi **a**siyezungumza anasoma | - | Shangazi **wa**siozungumza wanasoma. |



## Ulemavu

Binadamu huzaliwa au hupatwa na hali tofauti za kimaumbile. Wengine huzaliwa na ulemavu. Kuna walemavu wasioona na wale wasiosikia wala kuzungumza. Walemavu wengine huchechemea na wengine hutumia viti vya magurudumu. Wakati mwingine walemavu huhitaji usaidizi. Kwa mfano, tunaweza kuwasaidia kuvuka barabara na kwa kuwasomea hadithi. Ulemavu sio kutojiweza. Walemavu wamefanikiwa sana maishani mwao.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **u le ma vu - ulemavu**

★


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a | nu | ha | u | o | le |
| ka | ndu | ba | dhi | wa | si |
| ma | ki | vu | chwa | ti | na |

Sarufi: Soma maneno haya.

●

| **Neno** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| cheza | - | **usi**cheze |
| adhibu | - | **usi**adhibu |
| sikiza | - | **usi**sikize |
| ficha | - | **usi**fiche |
| fichua | - | **usi**fichue |

## Nandutu



Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| ma a gi zo | lo we sha | ku na wa |
| **maagizo** | **lowesha** | **kunawa** |
| ku gu sa | vi ga nja | se ku nde |
| **kugusa** | **viganja** | **sekunde** |
| vi do le | m sa la ni | sa bu ni |
| **vidole** | **msalani** | **sabuni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| u ji panguse | ku dumisha |
| **ujipanguse** | **kudumisha** |
| ku nawa | u ki tumia |
| **kunawa** | **ukitumia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-angu** | | **-ako** |
|---|---|---|
| Afya **yangu** ni nzuri | - | Afya **yako** ni nzuri. |
| Sabuni **yangu** ni nyeupe | - | Sabuni **yako** ni nyeupe. |
| Maji **yangu** ni safi | - | Maji **yako** ni safi. |
| Taulo **yangu** imezeeka | - | Taulo **yako** imezeeka. |



## Maagizo ya kunawa mikono

Kunawa mikono ni muhimu kwa afya yako. Ni muhimu kunawa mikono kabla ya kula au kugusa chakula, baada ya kwenda msalani, na baada ya kucheza. Fuata hatua hizi:

1. Hakikisha unatumia maji safi na sabuni.
2. Lowesha mikono kwa maji, kisha paka sabuni.
3. Tengeneza povu kisha lieneze kwenye viganja na katikati ya vidole.
4. Sugua mikono kwa muda wa sekunde kumi na tano.
5. Nawa kwa maji safi kisha ujipanguse kwa taulo safi.

Usafi ni mojawapo ya njia za kudumisha afya bora.

Soma silabi na maneno.

ma zi ngi ra
**mazingira**

ku u mwa
**kuumwa**

ki pi ndu pi ndu
**kipindupindu**

ma tu mbo
**matumbo**

ma go njwa
**magonjwa**

wa li zi bu a
**walizibua**

Soma sehemu za neno na neno lote.

★ a li zungumza
**alizungumza**

a li endelea
**aliendelea**

a li tu shauri
**alitushauri**

a li tu shukuru
**alitushukuru**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆ **Kuakifisha**

Kwa nini chakula kiliungua?

Kwa nini tunawe mikono kabla ya kula?

Kwa nini tunavaa sweta wakati wa baridi?

Kwa nini tunapaswa kula chakula safi?



## Usafi wa mazingira

Ijumaa asubuhi Mwalimu Mkuu, Bibi Kulamo, alizungumza kuhusu usafi wa mazingira ya shule yetu. Alisema mazingira yakiwa machafu tunaweza kupatwa na magonjwa. Alitushauri tusicheze kwenye nyasi ndefu kwani tunaweza kuumwa na nyoka au wadudu wabaya. Nyasi huficha wadudu kama mbu ambao huleta malaria. Aliendelea kusema kuwa kutupa takataka ovyoovyo pia ni hatari. Taka na maji machafu mitaroni yanaweza kutuletea magonjwa kama kipindupindu na homa ya matumbo. Baadaye, Bibi Kulamo alitupa kazi ya kufyeka nyasi na kuokota takataka. Baadhi ya wanafunzi walizibua mitaro iliyokuwa imezibika. Bibi Kulamo alitushukuru kwa kazi nzuri.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m ku ki - mkuki**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| mi | ma | ta | ri | pi |
| jo | ja | ba | chu | to |
| di | ka | vu | ku | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| -angu | | -ako |
|---|---|---|
| Afya **yangu** imeimarika | - | Afya **yako** imeimarika. |
| Maji **yangu** ni moto | - | Maji **yako** ni moto. |
| Mwalimu **wangu** ni mpole | - | Mwalimu **wako** ni mpole. |
| Mtoto **wangu** amefika | - | Mtoto **wako** amefika. |

## Ugonjwa wa kipindupindu



Soma silabi na maneno.

m cha nga nyi ko
**mchanganyiko**

mi ho go
**mihogo**

mbo ga
**mboga**

ma tu nda
**matunda**

ma ha ra gwe
**maharagwe**

ku je nga
**kujenga**

Soma sehemu za neno na neno lote.

ku hakikisha
**kuhakikisha**

i na pata
**inapata**

ku imarisha
**kuimarisha**

vya kula
**vyakula**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Chakula** hiki ni **kitamu** | - | **Vyakula** hivi ni **vitamu**. |
| **Chuma** hiki ni **kikubwa** | - | **Vyuma** hivi ni **vikubwa**. |
| **Choo** hiki ni **kichafu** | - | **Vyoo** hivi ni **vichafu**. |
| **Chombo** hiki ni **kizuri** | - | **Vyombo** hivi ni **vizuri**. |
| **Chungu** hiki ni **kidogo** | - | **Vyungu** hivi ni **vidogo**. |



## Lishe bora

Vyakula ni muhimu sana katika mwili wa binadamu. Ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kuwa jamii yake inapata lishe bora. Lishe bora ni mchanganyiko wa vyakula vya kujenga mwili, vya kuupa mwili nguvu na vile vya kuimarisha kinga mwilini. Vyakula vya kujenga mwili ni kama vile nyama, maharagwe na mayai. Vile vya kuupa mwili nguvu ni kama mihogo, mchele na ugali. Vyakula vya kusaidia kuzuia magonjwa ni kama mboga na matunda.

Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| go do ro | fo ro nya | m pi shi |
| **godoro** | **foronya** | **mpishi** |
| m si cha na | m ku li ma | nyo ro ro |
| **msichana** | **mkulima** | **nyororo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ni nunulia | ni ji tayarishe |
| **alininunulia** | **nijitayarishe** |
| ni ka badilika | ni li kuwa |
| **nikabadilika** | **nilikuwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja - ake** | | **Wingi - ao** |
|---|---|---|
| Mkulima **wake** ana bidii | - | **Wa**kulima **wao** wana bidii. |
| Mwashi **wake** amemaliza kazi | - | **Wa**ashi **wao** wamemaliza kazi. |
| Mpishi **wake** anapika vizuri | - | **Wa**pishi **wao** wanapika vizuri. |
| Mwandishi **wake** anapendeza | - | **Wa**andishi **wao** wanapendeza. |



## Ndoto na kazi

Siku chache zilizopita baba yangu alininunulia godoro na foronya nyororo. Jana usiku nilipolala niliota ndoto. Ndoto yangu ilikuwa hivi: Nilikuwa msichana mkubwa. Nilikuwa nimepata kazi ya ualimu. Baada ya kufanya kazi hiyo kwa muda, nilibadilika kuwa mkulima. Kwenye shamba langu kulikuwa na mboga nzuri za kijani na nyanya zilizoiva. Mbuzi wakaja na kula mboga zote. Nililia mpaka nikabadilika kuwa mpishi. Baadaye nilipika chakula kitamu sana. Watu walikula na kufurahi sana.
Hapo ndipo mama alipokuja na kuniamsha ili nijitayarishe kwenda shuleni.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m bu ni - mbuni**


★

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| pu | ta | de | wa | nya | u | twi |
| si | ni | mbu | ma | ga | me | nda |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Twiga **huyu** ni **m**refu | - | Twiga **hawa** ni **wa**refu. |
| Punda **huyu** ni **m**nono | - | Punda **hawa** ni **wa**nono. |
| Tausi **huyu ana** maringo | - | Tausi **hawa wa**na maringo. |
| Mbuni **huyu** **ana**furahisha | - | Mbuni **hawa** **wa**nafurahisha. |

## Wanyama dukani



Soma silabi na maneno.

| | |
|---|---|
| nde ge | ba ta m zi nga |
| **ndege** | **batamzinga** |
| ma nyo ya | f la mi ngo |
| **manyoya** | **flamingo** |
| ma ba wa | m si tu ni |
| **mabawa** | **msituni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa me changia | wa na po zuru |
| **wamechangia** | **wanapozuru** |
| wa na o fugwa | hu tu letea |
| **wanaofugwa** | **hutuletea** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| -haya | | -yale |
|---|---|---|
| Mabawa **haya** ni mapana | - | Mabawa **yale** ni mapana. |
| Manyoya **haya** ni marefu | - | Manyoya **yale** ni marefu. |
| Mayai **haya** ni madogo | - | Mayai **yale** ni madogo. |
| Mapato **haya** ni machache | - | Mapato **yale** ni machache. |



## Umuhimu wa ndege

Ndege au nyuni ni kiumbe chenye mabawa na manyoya. Ndege wengine hupatikana nyumbani na wengine msituni. Ndege wanaofugwa nyumbani ni kama kuku, bata na batamzinga. Ndege hawa hutupatia nyama na mayai. Ndege wa msituni ni kama vile mbuni, tausi na kanga. Ndege wanaoishi majini ni kama vile bata bukini na flamingo au heroe. Ndege hawa wamechangia sana katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Watalii wengi huja kuwaona ndege na wanyama.Wanapozuru nchi yetu wao hutuletea pesa za kigeni.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| tu mbi li | ma ga nda | so kwe |
| **tumbili** | **maganda** | **sokwe** |
| nge de re | mi a yo | m nya ma |
| **ngedere** | **miayo** | **mnyama** |
| mi me a | ma tu nda | wa du du |
| **mimea** | **matunda** | **wadudu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


★

| | |
|---|---|
| a na ye patikana | wa na o fanana |
| **anayepatikana** | **wanaofanana** |
| a na ye karibia | wa na po tafuta |
| **anayekaribia** | **wanapotafuta** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **Wakati uliopita (jana)** | **Wakati uliopo (sasa)** | **Wakati ujao (kesho)** |
|---|---|---|
| Mbwa **ali**patikana | **ana**patikana | **ata**patikana |
| Mgeni **ali**karibia | **ana**karibia | **ata**karibia |
| Babu **ali**ishi | **ana**ishi | **ata**ishi |
| Mwalimu **ali**tafuta | **ana**tafuta | **ata**tafuta |



## Tumbili

Je, wajua kwamba tumbili ni mnyama anayepatikana sehemu nyingi za dunia? Jina lingine la tumbili ni ngedere au kima. Tumbili ni mnyama anayekaribia mwanadamu kimaumbile na kwa tabia. Baadhi ya tabia hizi ni kama kula ndizi baada ya kuambua na kutupa maganda yake. Vilevile tumbili huishi na kusafiri pamoja. Wao hushirikiana wanapotafuta chakula. Tumbili hula vyakula kama vile: matunda, mimea ya majani na wadudu. Wanyama wengine wanaofanana na tumbili ni nyani na sokwe. Tumbili anapopiga miayo huwa amechoka au amekasirika.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nde ge - ndege**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ta | nde | tu | nya | ba |
| ki | i | fa | ku | ri |
| mbi | ni | wa | ge | du |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Wakati uliopita | Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|---|
| a**li**fanana | a**na**fanana | a**ta**fanana |
| a**li**zuru | a**na**zuru | a**ta**zuru |
| a**li**taga | a**na**taga | a**ta**taga |
| a**li**kimbia | a**na**kimbia | a**ta**kimbia |
| a**li**hama | a**na**hama | a**ta**hama |

## Ndege



Soma silabi na maneno.

ma u mbo
**maumbo**

pe mbe ta tu
**pembetatu**


du a ra du fu
**duaradufu**

du a ra
**duara**


m s ta ti li
**mstatili**


m ra ba
**mraba**


Aina ya maumbo


**mraba**


**mstatili**


**duaradufu**


**mviringo au duara**


**pembetatu**

Soma sehemu za neno na neno lote.

ya na pendeza
**yanapendeza**

hu onekana
**huonekana**

ya na staajabisha
**yanastaajabisha**

zi ki meta meta
**zikimetameta**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo** | **Wakati uliopita** |
|---|---|
| Maumbo haya ya**na**pendeza | - Maumbo yale ya**li**pendeza. |
| Maumbo haya ya**na**staajabisha | - Maumbo yale ya**li**staajabisha. |
| Maumbo haya ya**na**patikana | - Maumbo yale ya**li**patikana. |
| Maumbo haya ya**na**metameta | - Maumbo yale ya**li**metameta. |



## Maumbo

Maumbo yako kila mahali. Maumbo mengine yanapendeza na mengine yanastaajabisha. Zawadi inaweza kuwekwa katika sanduku lenye umbo la mraba. Tairi za baiskeli yangu na magurudumu ya gari ni ya umbo la duara. Meza na mlango wetu una umbo la mstatili. Mayai nayo yana umbo la duaradufu. Baadhi ya pakiti za maziwa zina umbo la pembetatu. Nyota ambazo huonekana usiku zikimetameta huwa na pembe nyingi.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m cho ro | m ra ba | ke nge le |
| **mchoro** | **mraba** | **kengele** |
| m vi ri ngo | sa mbu sa | sa ha ni |
| **mviringo** | **sambusa** | **sahani** |
| m s ta ti li | wa cho re | mwa li mu |
| **mstatili** | **wachore** | **mwalimu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.


★

| | |
|---|---|
| wa li vi kusanya | a li wa ambia |
| **walivikusanya** | **aliwaambia** |
| a li wa chorea | a li tangulia |
| **aliwachorea** | **alitangulia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

◆

| **wakati uliopita -li** | | **wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Wa**li**chora picha | - | Wa**ta**chora picha. |
| Wa**li**kuwa nyumbani | - | Wa**ta**kuwa nyumbani. |
| A**li**weka bakuli | - | A**ta**weka bakuli. |
| A**li**tangulia kanisani | - | A**ta**tangulia kanisani. |



## Kuchora maumbo

Asubuhi, wanafunzi wa darasa la pili walichora maumbo. Mwalimu aliwaambia wachore sahani. Chini ya mchoro huu wakaandika neno mviringo. Tena aliwaambia wachore kitabu ambacho pande zote ni sawa kwa urefu. Chini ya mchoro huu waliandika neno mraba. Mchoro wa tatu ulikuwa wa meza. Chini ya mchoro huu mwalimu aliandika neno mstatili. Kisha aliwaambia wachore yai. Chini ya mchoro waliandika neno duaradufu. Mwishowe aliwaambia wanafunzi wachore sambusa. Wanafunzi walishangaa, “Sambusa?” Mwalimu aliwachorea sambusa kwenye ubao. Chini ya mchoro huu aliandika neno pembetatu.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **du a ra - duara**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| m | a | ta | fu | pe |
| du | sta | ra | li | za |
| ka | mbe | ti | tu | du |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Wakati uliopo -na-**
Waimbaji wa**na**cheka
Wavuvi wa**na**msalimia
Waumini wa**na**enda

**Wakati ujao -ta-**
- Waimbaji wa**ta**cheka.
- Wavuvi wa**ta**msalimia.
- Waumini wa**ta**enda.

## Vitendawili

1. Kafunua jicho jekundu.
2. Tunamsikia lakini hatumwoni.
3. Paarrrr hadi Meka.
4. Ndege wangu abembea mlingotini.
5. Mwanangu analia mwituni.
6. Popote niendapo hunifuata.
7. Dadangu akitoka kwao harudi tena.
8. Mchana yuko usiku simwoni.
9. Chang'aa chapendeza lakini hakifikiwi.
10. Kamba ndefu lakini haifungi kuni.
11. Mzee kobe akilia watu hufurahi.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **kivuli** | **shoka** | **mvua** | **barabara** | **upepo** | **utelezi** |
| **kivuli** | **jua** | **upinde wa mvua** | | **maji ya mvua** | **bendera** |

Soma silabi na maneno.


| ha ta ri | ma tu mbo | m du du |
|---|---|---|
| **hatari** | **matumbo** | **mdudu** |
| ho ma | ki nga | u cha fu |
| **homa** | **kinga** | **uchafu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| a na po ishi | ki na po bakia |
|---|---|
| **anapoishi** | **kinapobakia** |
| ya na yo letwa | wa si ki chafue |
| **yanayoletwa** | **wasikichafue** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Ch**akula cha Ali ni **ki**chafu | - | **Vy**akula vya Ali ni **vi**chafu. |
| Nekesa ana **ch**akula safi | - | Nekesa ana **vy**akula safi. |
| Otieno anakula **ch**akula **ki**tamu | - | Otieno anakula **vy**akula **vi**tamu. |
| Juma alitupa **ch**akula **ki**baya | - | Juma alitupa **vy**akula **vi**baya. |



## Nzi

Nzi ni mdudu hatari sana kwa maisha ya binadamu. Mdudu huyu hupenda uchafu sana. Yeye husababisha magonjwa kama vile kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Kwa hivyo ni muhimu kila mtu ahakikishe kuwa mahali anapoishi ni safi. Kinga ni bora kuliko tiba. Kwa hivyo ni bora kujikinga kutokana na magonjwa yanayoletwa na nzi. Nyumbani na shuleni pia ni lazima kuwe safi. Chakula kinapobakia ni muhimu kifunikwe ili nzi wasikichafue.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| m sa la ni | ha ru fu | vi o shwe |
| **msalani** | **harufu** | **vioshwe** |
| u sa fi | ku du mi sha | vyo o |
| **usafi** | **kudumisha** | **vyoo** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li tu tembelea | wa li m tambua |
| **alitutembelea** | **walimtambua** |
| tu li m karibisha | ku wa shauri |
| **tulimkaribisha** | **kuwashauri** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| Kamau **ameketi** | - | Kamau **amesimama**. |
| **Kuja hapa** | - | **Enda pale**. |
| Kendi **amevaa** sweta | - | Kendi **amevua** sweta. |
| Kikombe kiko **chini ya** meza | - | Kikombe kiko **juu ya** meza. |
| Nyumba hii ni **safi** | - | Nyumba hii ni **chafu**. |
| Dengu hizi ni **chache** | - | Dengu hizi ni **nyingi**. |



## Mama Safi shuleni

Mama Safi alitutembelea shuleni Bondeni. Tulimkaribisha kwa furaha. Alipoketi chini, sherehe ikaanza. Mama Safi alihisi furaha sana. Bila kusema jina lake, watu walimtambua kwa sababu ya mavazi yake. Alipopewa nafasi kuihutubia halaiki alisema, "Mwalimu Mkuu, Bwana Bakari, walimu na wanafunzi, hamjambo? Leo nimekuja kuwashauri kuhusu usafi wa vyoo vyetu. Shuleni au nyumbani, vyoo ni lazima vioshwe vizuri kila siku. Njia moja ya kudumisha usafi ni kuhakikisha kwamba vyoo havina harufu wala wadudu wabaya." Mama Safi alimalizia kwa kusema, "Mnapoenda msalani, ni muhimu mvae viatu. Pia ni lazima mnawe mikono kwa sabuni baada ya kuutumia msala. Mkifanya hivyo bila shaka mtakuwa na afya njema."

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nya ni - nyani**


★

| | | | |
|---|---|---|---|
| mbo | ge | nya | bu |
| i | te | mba | ka |
| nde | m | si | ni |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Hiki ni **ki**atu **cha**ngu | - | Hivi ni **vi**atu **vye**tu. |
| Hiki ni **ki**atu **cha**ko | - | Hivi ni **vi**atu **vye**nu. |
| Hiki ni **ki**tabu **cha**ngu | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**tu. |
| Hiki ni **ki**tabu **cha**ko | - | Hivi ni **vi**tabu **vye**nu. |

## Tembo asaidiwa



# Kazi mbalimbali

Soma silabi na maneno.

ma fu mbo
**mafumbo**

ho s pi ta li ni
**hospitalini**

m ku li ma
**mkulima**

sha mba ni
**shambani**

da k ta ri
**daktari**

se re ma la
**seremala**

Soma sehemu za neno na neno lote.

zi na zo fanywa
**zinazofanywa**

wa li furahia
**walifurahia**

hu wa hudumia
**huwahudumia**

ku tengeneza
**kutengeneza**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nili**enda sokoni | - | **Siku**enda sokoni. |
| **Nili**tumia sabuni | - | **Siku**tumia sabuni. |
| **Nili**uza makaa | - | **Siku**uza makaa. |
| **Nili**fanya kazi ya ziada | - | **Siku**fanya kazi ya ziada. |



## Mafumbo ya Kazi

Yusufu, Owalo na Linda walisema mafumbo kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na watu. Yusufu aliuliza, "Mimi hupanda mimea kama mahindi na mboga shambani. Je, mimi ni nani?" Linda alijibu, "Mkulima." Owalo naye aliuliza, "Mimi huwahudumia wagonjwa hospitalini. Je, mimi ni nani?" Yusufu alijibu, "Daktari." Linda pia aliuliza, "Mjomba wangu hufanya kazi ya kutengeneza vitu kwa kutumia mbao. Je, yeye ni nani?" Yusufu na Owalo walijibu pamoja, "Fundi!" Linda alisema, "Mmenoa. Nipeni mji nitawapa jibu sahihi." Yusufu alimpa mji wa Mombasa. Linda alisema, "Nilienda Mombasa, watu wa Mombasa wakasema jibu ni seremala." Wote walifurahishwa na mafumbo hayo.

Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| ku u za | ma kaa | ge si |
| **kuuza** | **makaa** | **gesi** |
| po li si | f ri ji | su fu ri a |
| **polisi** | **friji** | **sufuria** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ni li li nunua | a li wa pigia |
| **nililinunua** | **aliwapigia** |
| ku m kamata | a li shtuka |
| **kumkamata** | **alishtuka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **wakati uliopita -li** | **wakati uliopo -na** |
|---|---|
| Mteja a**li**fanya hesabu | - Mteja a**na**fanya hesabu. |
| Msafiri a**li**fika dukani | - Msafiri a**na**fika dukani. |
| Muuzaji a**li**ibiwa na wezi | - Muuzaji a**na**ibiwa na wezi. |
| Mwanamke a**li**wapigia simu polisi | - Mwanamke a**na**wapigia simu polisi. |



## Swaleh ashikwa na polisi

Swaleh alifanya kazi ya kuuza vitu dukani. Duka lake lilikuwa na bidhaa mbalimbali. Kati ya vitu alivyouza ni viti vya kukalia au sofa, sufuria, pasi, jiko la makaa na friji. Siku moja Atieno alifika kwenye duka la Swaleh. Alishtuka kuliona jiko lake la gesi ambalo lilikuwa limeibwa siku chache zilizopita. Bila kupoteza wakati Atieno aliwapigia polisi simu. Polisi walifika mara moja na kumkamata Swaleh. Swaleh akajitetea kwa kusema, “Mimi sina makosa. Jiko hili nililinunua kutoka kwa mtu nisiyemjua.”

# Kazi mbalimbali

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **de re va - dereva**


★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| la | ma | hu | si | nzi | se |
| ndi | na | re | pi | de | ku |
| fu | li | su | m | shi | va |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **Nili**fanya kazi zote | - | **Siku**fanya kazi zote. |
| **Nili**pika chai | - | **Siku**pika chai. |
| **Nili**wahudumia wagonjwa | - | **Siku**wahudumia wagonjwa. |
| **Nili**wapigia simu | - | **Siku**wapigia simu. |

## Fundi Mukundi



Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| A go s ti | O k to ba | De se mba |
| **Agosti** | **Oktoba** | **Desemba** |
| Fe b ru a ri | Ja nu a ri | Se p te mba |
| **Februari** | **Januari** | **Septemba** |
| A p ri li | Ju ni | Ju la i |
| **Aprili** | **Juni** | **Julai** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu tu karibisha | hu ni furahisha |
| **hutukaribisha** | **hunifurahisha** |
| tu na agana | hu zingatia |
| **tunaagana** | **huzingatia** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| mwaka mmoja | - | miaka miwili |
| mwezi mmoja | - | miezi miwili |
| muhula mmoja | - | mihula miwili |
| mtihani mmoja | - | mitihani miwili |
| mwili mmoja | - | miili miwili |



## Miezi ya mwaka

Mwaka mmoja huwa na miezi kumi na miwili. Januari hutukaribisha shuleni. Februari na Machi ni kucheza na kuendelea kujuana na wenzetu. Aprili hunitia woga kwani tunaagana na marafiki zangu. Mei, Juni na Julai hunifurahisha. Huwa ni miezi ya kukutana na marafiki zangu tena. Hadithi za likizo nazo huwa nyingi. Agosti mimi hurudi nyumbani kungojea Septemba. Oktoba mimi huzingatia masomo kwani Novemba mtihani waningojea. Desemba mimi hupungia darasa mkono wa buriani kwani nasonga mbele.

Soma silabi na maneno.

ma va zi

**mavazi**

vi nywa ji

**vinywaji**

Wa k ri s to

**Wakristo**

ma chu ngwa

**machungwa**

i shi ri ni

**ishirini**

she re he

**sherehe**

Soma sehemu za neno na neno lote.

tu na po karibia

**tunapokaribia**

hu ni nunulia

**huninunulia**

hu kumbukwa

**hukumbukwa**

hu tu peleka

**hutupeleka**

Sarufi: Soma sentensi hizi.


**Kuakifisha**

Hiki ni kinywaji kitamu.

Kwa nini kinywaji ni kitamu?

Kwa nini kikombe kilivunjika?

Kikombe kilivunjika.




## Mwezi wa Disemba

Naupenda mwezi wa Disemba. Mwezi huu hukumbukwa na Wakristo kote duniani. Ni mwezi wa kukumbuka siku ya Yesu Kristo kuzaliwa.Tunapokaribia Disemba wazazi wangu huninunulia mavazi mazuri. Baba hutupeleka kutembelea miji mbalimbali. Tarehe ishirini na tano, sisi hupika vyakula vitamu kama vile chapati, wali, kuku na nyama. Baada ya kuvila sisi huviteremsha kwa vinywaji kama soda na maji ya machungwa. Sherehe hizi huwa za kufana sana.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **Me i - Mei**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ri | fe | sti | mba | ma |
| se | go | l | ua | ri |
| a | ju | de | la | chi |
| ni | ja | nu | me | br |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo -na** | | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Watoto wa**na**cheka | - | Watoto wa**ta**cheka. |
| Watu wa**na**enda | - | Watu wa**ta**enda. |
| Wazee wa**na**msalimia | - | Wazee wa**ta**msalimia. |
| Wakulima wa**na**pata | - | Wakulima wa**ta**pata. |

## Kibuyu cha ajabu



Soma silabi na maneno.

mwa nga li fu
**mwangalifu**

wa nya ma
**wanyama**

ki vu ki o
**kivukio**

a ja li
**ajali**

de re va
**dereva**

ho s pi ta li
**hospitali**










Soma sehemu za neno na neno lote.

ku wa fahamisha
**kuwafahamisha**

wa na o tumia
**wanaotumia**

i na yo onyesha
**inayoonyesha**

zi na po fuatwa
**zinapofuatwa**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Lile ni **ga**ri refu | - | Yale ni **ma**gari **ma**refu. |
| Lile ni **ga**ri kubwa | - | Yale ni **ma**gari **ma**kubwa. |
| Lile ni **ga**ri chafu | - | Yale ni **ma**gari chafu. |
| Lile ni **ga**ri safi | - | Yale ni **ma**gari safi. |




## Alama za barabarani

Alama za barabarani ni muhimu kwa watu wote wanaotumia barabara. Watu wote wanaotembea kwa miguu, wale wanaoendesha baiskeli na madereva wa magari wanastahili kuzingatia alama hizo. Alama ya kivukio cha watoto huwekwa karibu na shule ili kuwafahamisha wanaotumia barabara kuwa waangalifu. Ni hatari watoto kucheza au kukimbizana barabarani. Alama nyingine ni herufi **H** inayoonyesha hospitali. Dereva anapofika hapo ni lazima awe mwangalifu. Vilevile, hapaswi kupiga honi ovyoovyo karibu na shule au hospitali. Alama zingine ni kama kivukio cha wanyama na kivukio cha watu. Alama na sheria za barabarani zinapofuatwa hupunguza ajali.

# Alama za barabarani

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| Ra shi di | de re va | t ra fi ki |
| **Rashidi** | **dereva** | **trafiki** |
| s ta di | m zu ngu ko | nye ku ndu |
| **stadi** | **mzunguko** | **nyekundu** |











Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ha ku hitimu | a li m danganya |
| **hakuhitimu** | **alimdanganya** |
| a li ji fundisha | i li yo fuata |
| **alijifundisha** | **iliyofuata** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Wakati uliopo -na** | | **Wakati ujao -ta** |
|---|---|---|
| Dereva huyu a**na**hitimu | - | Dereva huyu a**ta**hitimu. |
| Rashidi a**na**julikana sana | - | Rashidi a**ta**julikana sana. |
| Mtu huyu a**na**mdanganya | - | Mtu huyu a**ta**mdanganya. |
| Roda a**na**shangaa sana | - | Roda a**ta**shangaa sana. |



## Dereva Rashidi

Rashidi alikuwa dereva ambaye hakuhitimu. Alijifundisha kuendesha gari kijijini. Siku moja Rashidi alimtembelea shangazi yake mjini Nairobi. Alipofika huko alimdanganya kwamba yeye ni dereva stadi. Shangazi yake alifurahi sana. Alijua sasa ingekuwa rahisi kwake yeye kwenda soko la Marikiti kila siku. Asubuhi iliyofuata shangazi aliamua kuenda sokoni. Rashidi aliruka kwenye gari harakaharaka ili kuliendesha. Walipofika kwenye mzunguko wa magari, Rashidi hakujua umuhimu wa taa za trafiki. Huyo! Alifululiza moja kwa moja japo aliiona taa nyekundu. Shangazi alishangaa! Kufumba na kufumbua macho, waliligonga gari lingine.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ma ta tu - matatu**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| la | ma | ri | si | ba | mo |
| ta | pi | ki | shi | tu | ga |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

- **Umoja -ako** — **Wingi -enu**

Hili ni gari **lako** - Haya ni **ma**gari **yenu**.
Hili ni koti **lako** - Haya ni **ma**koti **yenu**.
Hili ni basi **lako** - Haya ni **ma**basi **yenu**.
Hili ni pipa **lako** - Haya ni **ma**pipa **yenu**.

## Ufalme wa kobe



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| mi tu mbwi | ba i s ke li | wa na ma ji |
| **mitumbwi** | **baiskeli** | **wanamaji** |
| e ro ple ni | ma no wa ri | u sa fi ri |
| **eropleni** | **manowari** | **usafiri** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li tumia | u me endelea |
| **walitumia** | **umeendelea** |
| wa li tembea | hu tumiwa |
| **walitembea** | **hutumiwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja (yako)** | | **Wingi (zenu)** |
|---|---|---|
| Meli **yako** imeenda | - | Meli **zenu** zimeenda. |
| Feri **yako** imechafuka | - | Feri **zenu** zimechafuka. |
| Manowari **yako** imezama | - | Manowari **zenu** zimezama. |
| Baiskeli **yako** imeharibika | - | Baiskeli **zenu** zimeharibika. |




## Usafiri

Zamani za kale, watu walitumia njia tofauti za usafiri. Watu wengi walitembea muda mrefu kwa miguu. Wengine walitumia wanyama kwa usafiri wao na wa mizigo pia. Watu walioishi karibu na mito, bahari na maziwa walitumia dau na mitumbwi. Mbali na kutembea, siku hizi watu wanatumia aina mbalimbali za magari, eropleni, baiskeli na pikipiki. Usafiri wa majini pia umeendelea sana. Siku hizi kuna meli, feri na manowari. Manowari hutumiwa sana na majeshi ya wanamaji vitani.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| du me | bu ndi | ma pa mbo |
| **dume** | **bundi** | **mapambo** |
| ta u si | u shu ngi | chi ri ku |
| **tausi** | **ushungi** | **chiriku** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ya na yo tumika | ku burudisha |
| **yanayotumika** | **kuburudisha** |
| hu tofautiana | ku pendeza |
| **hutofautiana** | **kupendeza** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Ndege huyu ana **m**domo mrefu | - Ndege hawa wana **mi**domo mirefu. |
| Anatuonyesha **m**fano mzuri | - Wanatuonyesha **mi**fano mizuri. |
| Chiriku huyu **ana** sauti nzuri | - Chiriku hawa **wana** sauti nzuri. |
| Nyuni huyu **ana** sauti nyororo | - Nyuni hawa **wana** sauti nyororo. |
| Tausi huyu **ana** rangi nzuri | - Tausi hawa **wana** rangi nzuri. |



## Maumbile ya ndege

Ndege wengi hutofautiana kimaumbile. Utaona tofauti kati ya ndege mbalimbali hata baina ya dume na jike wa aina moja. Kwa mfano, tausi dume ana rangi nzuri kuliko jike. Njiwa jike huwa na mdomo mrefu kuliko njiwa dume. Bundi jike ana shingo nyembamba na dume ana shingo nene.

Baadhi ya ndege pia huwa na ushungi juu ya vichwa vyao na wengi hawana.

Ndege pia wana manyoya mazuri ya kupendeza. Kwa mfano, tausi na kanga wana manyoya yanayotumika kama mapambo. Ndege wana sauti tofauti za kuburudisha. Nyimbo za ndege huwa na ujumbe fulani. Watu wengi huamini kuwa chiriku ana sauti nzuri kuliko ndege wengine.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **fe ri - feri**


★

| | | | |
|---|---|---|---|
| fe | da | li | ri |
| pi | nwa | mi | ma |
| me | gu | ga | ki |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Sentensi | Hali ya kukanusha |
|---|---|
| **Wali**tumia machela | - **Hawa**kutumia machela. |
| **Wali**tembea kwa miguu | - **Hawa**kutembea kwa miguu. |
| **Wali**ishi mjini | - **Hawa**kuishi mjini. |
| **Wali**tofautiana | - **Hawa**kutofautiana. |

## Ugonjwa wa malaria



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ja wa bu | nye u si | wa ri di |
| **jawabu** | **nyeusi** | **waridi** |
| nye ku ndu | sa ma wa ti | u fu o ni |
| **nyekundu** | **samawati** | **ufuoni** |


Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| u si staajabu | ku pendeza |
| **usistaajabu** | **kupendeza** |
| li ki chomoza | ni ta li jibu |
| **likichomoza** | **nitalijibu** |

Sarufi: Soma sentensi hizi

**Matumizi ya -angu na -etu**

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Hili ni kaa **langu** | - | Haya ni **ma**kaa **yetu**. |
| Hili ni swali **langu** | - | Haya ni **ma**swali **yetu**. |
| Hili ni ua **langu** | - | Haya ni **ma**ua **yetu**. |
| Hili ni jibu **langu** | - | Haya ni **ma**jibu **yetu**. |
| Hili ni pipa **langu** | - | Haya ni **ma**pipa **yetu**. |



## Rangi

Rangi zote za ajabu, leo takupa jawabu,
Maswali yote nitajibu, nawe usistaajabu.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Nyekundu ni rangi gani? Ya maua natangaza,
Ua waridi la kupendeza, na jua likichomoza.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Nyeusi ni rangi pia, ambayo najivunia
Ni rangi ya nywele zangu, iliyo nyeusi pia.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Samawati ni rangi gani? Ndio rangi ya angani,
Na maji ya baharini, kuogelea ufuoni.
**Rangi hupendeza macho, na pia zinavutia.**

Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | mwa nga za | ma to ne |
| **bendera** | **mwangaza** | **matone** |
| i ndi go | u ru ju a ni | ma nja no |
| **indigo** | **urujuani** | **manjano** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| li na po mulika | hu onekana |
| **linapomulika** | **huonekana** |
| u na po kutana | hu tawanyika |
| **unapokutana** | **hutawanyika** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Fulana **hii** ni nyekundu | - Fulana **hizi** ni nyekundu. |
| Nguo **hii** ni ya samawati | - Nguo **hizi** ni za samawati. |
| Kalamu **hii** ni nyeupe | - Kalamu **hizi** ni nyeupe. |
| Penseli **hii** ni nyeusi | - Penseli **hizi** ni nyeusi. |



## Rangi mbalimbali

“Je, unajua rangi za bendera yetu?” Babu aliuliza. “Ndiyo,” Kalu akajibu, “mwalimu wetu alituambia kuwa bendera yetu ina rangi nne. Juu huwa rangi ya urujuani kama shati langu. Katikati ni nyekundu kama damu na chini ni rangi ya kijani kibichi. Rangi hizo zimegawanywa kwa rangi ya manjano.” Babu akasema, “Samahani Kalu. Rangi iliyo juu katika bendera yetu ni nyeusi. Nayo inayozigawanya ni nyeupe kama karatasi hii. Rangi kama indigo ambayo inafanana na koti hili langu haipatikani katika bendera yetu.” “Asante babu. Sasa nimezifahamu rangi za bendera vyema,” Kalu akasema.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **sa ma wa ti - samawati**


★

| | | | |
|---|---|---|---|
| sa | nye | ma | ku |
| wa | si | ti | ndu |
| ni | uki | pe | ja |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| Maji **yali**poteza rangi | - | Maji **hayaku**poteza rangi. |
| Maji **yali**tapakaa kote | - | Maji **hayaku**tapakaa kote. |
| Maji **yali**sababisha madhara | - | Maji **hayaku**sababisha madhara. |

## Kwa nini mbingu ni samawati?



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| cho mbo | ki sa sa | ku fu ngwa |
| **chombo** | **kisasa** | **kufungwa** |
| ma u mbo | o fi si ni | shu ghu li |
| **maumbo** | **ofisini** | **shughuli** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| ku wekwa | hu tofautiana |
| **kuwekwa** | **hutofautiana** |
| i ta ku saidia | hu tumiwa |
| **itakusaidia** | **hutumiwa** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| Amesimama **karibu** na ukuta | - | Ameketi **mbali** na ukuta. |
| Kitabu kiko **juu** ya meza | - | Kitabu kiko **chini** ya meza. |
| Mlingoti uko **mbele** ya ofisi | - | Mlingoti uko **nyuma** ya ofisi. |
| Kitanda kiko **ndani** ya nyumba | - | Kitanda kiko **nje** ya nyumba. |




## Saa

Saa ni chombo cha kupimia muda au wakati. Kuna saa za kufungwa mkononi. Hizi huwa ndogo kiasi lakini hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Kuna saa za kuwekwa ukutani. Hizi nazo hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Pia kuna saa za kuwekwa mezani. Hizi pia hutofautiana kwa maumbo na ukubwa. Saa za mkono hutumiwa na mtu mmoja. Saa za ukutani na mezani mara nyingi hutumiwa na watu wengi. Saa ni muhimu shuleni, ofisini, nyumbani na hata hospitalini. Ni vizuri kuwa na saa. Itakusadia kufanya shughuli zako za kila siku kwa wakati unaofaa.

Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| mwe ma | fo le ni | ma ra fiki |
| **mwema** | **foleni** | **marafiki** |
| wa ka ti | pa re di | a su bu hi |
| **wakati** | **paredi** | **asubuhi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| hu wa ongoza | hu ji tayarisha |
| **huwaongoza** | **hujitayarisha** |
| i na po wadia | i ta ku saidia |
| **inapowadia** | **itakusaidia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja (hii)** | **Wingi (hizi)** |
|---|---|
| Saa **hii** ni ya **mwa**nafunzi | - Saa **hizi** ni za **wa**nafunzi. |
| Ofisi **hii** ni ya **mwa**limu | - Ofisi **hizi** ni za **wa**limu. |
| Nyumba **hii** ni ya **m**zazi wangu | - Nyumba **hizi** ni za **wa**zazi wetu. |
| Shule **hii** ni ya msingi | - Shule **hizi** ni za msingi. |



## Mwema

Mwema huishi karibu na shule yake. Kila siku, yeye huamka saa kumi na mbili asubuhi. Bila kupoteza wakati, yeye hujitayarisha kwenda shuleni. Saa moja inapowadia, Mwema hupata kiamshakinywa. Yeye huanza safari yake kwenda shuleni. Saa mbili wanafunzi hupanga foleni kwenda paredi. Baada ya paredi wanafunzi hurudi darasani kuanza masomo. Mwalimu wao huwasalimia, "M hali gani wanafunzi?" Wao hujibu, "Njema." Saa nne kamili wao huenda kucheza nje na marafiki zao. Saa sita kamili, Mwema hurudi nyumbani. Kabla ya kwenda, mwalimu wao huwaongoza kuimba wimbo mtamu wa "**Nasikia Sauti**."

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **a su bu hi - asubuhi**


★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ma | na | su | ni | cha |
| a | cho | ku | bu | pe |
| ke | u | mi | o | si |
| ro | sa | ji | m | hi |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| Nguo **hii** ni nzuri | - | Nguo **hizi** ni nzuri. |
| Hospitali **hii** ni kubwa | - | Hospitali **hizi** ni kubwa. |
| Meza **hii** ni pana | - | Meza **hizi** ni pana. |
| Hadithi **hii** ni ndefu | - | Hadithi **hizi** ni ndefu. |

## Obura na saa yake



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku pe nde za | ma zi ngi ra | wa na ri a dha |
| **kupendeza** | **mazingira** | **wanariadha** |
| mbu ga | ma a ja bu | u li mwe ngu |
| **mbuga** | **maajabu** | **ulimwengu** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa me tu letea | ku tafuta |
| **wametuletea** | **kutafuta** |
| hu furahia | wa na hitaji |
| **hufurahia** | **wanahitaji** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **-etu** | | **-enu** |
|---|---|---|
| Wanariadha **wetu** wameshinda | - | Wanariadha **wenu** wameshinda. |
| Wanyama **wetu** ni muhimu sana | - | Wanyama **wenu** ni muhimu sana. |
| Watu **wetu** ni wazuri | - | Watu **wenu** ni wazuri. |
| Wachezaji **wetu** ni mashuhuri | - | Wachezaji **wenu** ni mashuhuri. |



## Nchi ya Kenya

Kenya ni nchi ya kupendeza sana. Wanariadha wetu wametuletea sifa ulimwenguni kwa ushindi wao katika mbio za masafa marefu. Watu wengi hufurahia kuzuru nchi ya Kenya.Watu kutoka mabara mengine huja kuwaona wanyama pori kwenye mbuga zetu. Jiji la Nairobi ni jiji la kipekee ulimwenguni. Jiji hili lina mbuga ya wanyama. Mlima Kenya ni wa pili kwa urefu katika milima yote barani Afrika. Mbuga ya Masai Mara ni mojawapo ya maajabu ya ulimwengu. Hii ni kwa sababu ya kongoni ambao huvuka mto Mara katika msimu wao kila mwaka. Ni desturi kwa wanyama hawa kuvuka kuja upande wa Kenya kutafuta malisho. Wanyama wanahitaji mazingira mema. Ili tupate faida kutokana na utalii, ni lazima tuyalinde mazingira yetu.

Soma silabi na maneno.

vyu ma
**vyuma**

m mo mo nyo ko
**mmomonyoko**

cha nga mo to
**changamoto**

mba o
**mbao**

p la s ti ki
**plastiki**

ka ra ta si
**karatasi**

Soma sehemu za neno na neno lote.

tu na vyo tumia
**tunavyotumia**

vi na po tupwa
**vinapotupwa**

hu tengenezwa
**hutengenezwa**

vi li vyo tengenezwa
**vililivyotengenezwa**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | **Kukanusha** |
|---|---|
| Vitu hivi **vina**oza | - Vitu hivi **havi**ozi. |
| Vyuma vile **vina**tupwa | - Vyuma vile **havi**tupwi. |
| Vizazi vya sasa **vina**lindwa | - Vizazi vya sasa **havi**lindwi. |
| Vitabu vyetu **vina**tumiwa | - Vitabu vyetu **havi**tumiwi. |



## Linda mazingira

Vitu vingi tunavyotumia kila siku hutengenezwa kwa vyuma, mbao, plastiki au hata chupa. Vitu hivi vinapotupwa, haviozi kwa urahisi. Hivyo basi changamoto kubwa tuliyo nayo ni kuepukana na kuharibu mazingira yetu. Ni muhimu kutupa takataka mahali panapofaa. Ni vyema pia kutumia vitu ambavyo vimetengenezwa kwa chupa, karatasi au chuma. Tujaribu kuepuka kutumia vitu vilivyotengenezwa kwa plastiki. Tuvitumie vitu hivi kwa muda mrefu kabla ya kuvitupa. Ni lazima pia tupande miti mingi tunavyoweza. Miti huboresha hewa, hupunguza mmomonyoko wa udongo na kuleta mvua. Kazi yetu ni kuyalinda mazingira yetu kwa vizazi vijavyo.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **m li ma - mlima**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| to | ti | nya | ki |
| m | di | mbu | ju |
| sa | mi | ma | ga |
| a | li | vu | ra |

Sarufi: Soma maneno haya.

| -etu | | -enu |
|---|---|---|
| watoto **wetu** | - | watoto **wenu** |
| wanyama **wetu** | - | wanyama **wenu** |
| wazazi **wetu** | - | wazazi **wenu** |
| walimu **wetu** | - | walimu **wenu** |
| ndege **wetu** | - | ndege **wenu** |

## Mwezi



Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| wa na ngu | ku cho ta | Ma ri a |
| **wanangu** | **kuchota** | **Maria** |
| ta fa dha li | na a mi ni | Ma ta no |
| **tafadhali** | **naamini** | **Matano** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| tu si achwe | a ta ni peleka |
| **tusiachwe** | **atanipeleka** |
| tu ki kamilisha | tu na shukuru |
| **tukikamilisha** | **tunashukuru** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| **Nina**umwa sana | - | **Si**umwi sana. |
| **Nina**baki hapa nyumbani | - | **Si**baki hapa nyumbani. |
| **Nina**msaidia mama yako | - | **Si**msaidii mama yako. |
| **Nina**piga simu kazini | - | **Si**pigi simu kazini. |
| **Nina**mpeleka mama hospitalini | - | **Si**mpeleki mama hospitalini. |



## Mchezo wa kuigiza: Mama augua

**Mama**: Wanangu, naumwa sana. Sijiwezi sijitambui. Inabidi niende kumwona daktari mara moja. Baba yenu atanipeleka.

**Baba**: Sijui kama nitapewa ruhusa kazini. Hebu nimpigie simu mkubwa wangu. Na wewe Maria tafadhali ukitoka shuleni leo, usaidie hapa nyumbani. Unaweza kusaidiana na Matano kuchota maji na kupika chakula.

**Maria**: Naam baba. Tunashukuru. Tukikamilisha kazi nyumbani tutasoma vitabu vyetu ili tusiachwe nyuma.

**Baba**: Ninaona mnapenda kusoma sana wanangu. Haya basi, nendeni.

**Matano**: Asante baba. Naamini mama atapata nafuu.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ka ti ba | ma e nde le o | u ta ma du ni |
| **katiba** | **maendeleo** | **utamaduni** |
| po to vu | dhu lu ma | ma dha ra |
| **potovu** | **dhuluma** | **madhara** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na zo tokana | ku wa saidia |
| **zinazotokana** | **kuwasaidia** |
| i na pinga | ku faidi |
| **inapinga** | **kufaidi** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Sentensi** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| Mila hizi ni **nzuri** | - | Mila hizi ni **mbaya.** |
| Jamii hii ni **kubwa** | - | Jamii hii ni **ndogo.** |
| Katiba hii ni ya **sasa** | - | Katiba hii ni ya **zamani.** |
| Madhara haya ni **makubwa** | - | Madhara haya ni **madogo.** |



## Mila na tamaduni

Kila jamii kote duniani ina utamaduni wake. Kuna baadhi ya mambo katika utamaduni ambayo ni potovu. Utamaduni mzuri hujenga na kufaidi jamii na watu binafsi. Utamaduni potovu huleta madhara katika maisha na maendeleo ya jamii. Baadhi ya mambo mazuri katika jamii ni kama vile watoto kutii wazazi wao na kuwasaidia kazi za nyumbani. Baadhi ya mambo potovu ni kama ndoa za mapema, tabia ya kuiba ng'ombe na vita kati ya jamii. Katiba ya Kenya inalinda kila mkenya. Inapinga utamaduni mbaya pamoja na dhuluma zinazotokana na utamaduni huo.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ka ti ba - katiba**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ma | ti | la | ka | mi | dhu |
| ba | cho | po | ba | mwe | ri |
| to | tu | ku | zi | che | vu |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | | Kukanusha |
|---|---|---|
| **ni**nacheka | - | **si**cheki |
| **ni**nalia | - | **si**lii |
| **ni**naimba | - | **si**imbi |
| **ni**nabeba | - | **si**bebi |
| **ni**nakata | - | **si**kati |

## Mavazi



Soma silabi na maneno.

u ta ma du ni — ma bu i bu i — wa ta wa

**utamaduni** **mabuibui** **watawa**

ki i sla mu — ma ri nda — wa ka to li ki

**kiislamu** **marinda** **wakatoliki**

Soma sehemu za neno na neno lote.

hu tofautiana — hu tumiwa

**hutofautiana** **hutumiwa**

hu valiwa — hu patikana

**huvaliwa** **hupatikana**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| **Hili** ni vazi fupi | - | **Haya** ni **ma**vazi **ma**fupi. |
| **Hili** ni rinda zuri | - | **Haya** ni **ma**rinda **ma**zuri. |
| **Hili** ni buibui refu | - | **Haya** ni **ma**buibui **ma**refu. |
| **Hili** ni shati dogo | - | **Haya** ni **ma**shati **ma**dogo. |



## Mavazi mbalimbali

Kuna mavazi mbalimbali ambayo huvaliwa na wanadamu. Mavazi haya hutofautiana kwa sababu ya utamaduni, dini, sherehe, kazi na hata hali ya anga. Kwa mfano, kanzu huvaliwa na wanaume wa dini ya kiislamu. Nao wanawake waislamu huvalia mabuibui. Watawa wa kikatoliki huvaa veli na marinda marefu. Kanga na shuka hutumiwa kama mavazi ya kitamaduni. Jina lingine la kanga ni leso na hupatikana katika rangi mbalimbali. Leso huwa na maandishi yenye ujumbe spesheli.

Soma silabi na maneno.


| | | |
|---|---|---|
| wa me vaa | ki le mba | nye u pe |
| **wamevaa** | **kilemba** | **nyeupe** |
| ka nzu | shu ka | vye u si |
| **kanzu** | **shuka** | **vye usi** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i li po wadia | a li ji funga |
| **ilipowadia** | **alijifunga** |
| a li mu uliza | wa li agana |
| **alimuuliza** | **waliagana** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Nipatie **ki**lemba **che**upe | - | Tupatie **vi**lemba **vye**upe. |
| Ninataka **ki**atu **che**kundu | - | Tunataka **vi**atu **vye**kundu. |
| Ninapenda **koti je**usi | - | Tunapenda **ma**koti **me**usi. |
| Ninavaa **r**inda **je**usi | - | Tunavaa **ma**rinda **me**usi. |



## Siku ya ibada

Siku ya Jumapili ilipowadia Mzee Okelo alivalia koti jeusi. Alijifunga kilemba chake kichwani na kuvalia viatu vyeusi. Alianza safari kuelekea kanisani. Njiani alikutana na rafiki yake Mzee Sakuda. Mzee Sakuda alikuwa amevaa kanzu nyeupe pepepe. “Mbona huendi kanisani leo?” Okelo alimuuliza rafiki yake. “Ninaenda kumwona shangazi yangu ambaye ameugua kwa muda mrefu,” alijibu Mzee Sakuda. Basi waliagana na Mzee Okelo akashika njia moja kwa moja hadi kanisani. Huko watu walikuwa wamevaa nguo za aina mbalimbali.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **sha ti - shati**

★


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| mba | nda | ri | sha | bui | a |
| li | re | ti | le | sa | rua |
| i | ke | su | nga | ki | bui |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

● **Umoja** — **Wingi**

Buibui **hili** ni chafu - **Ma**buibui **haya** ni **ma**chafu.
Shati **hili** ni refu - **Ma**shati **haya** ni **ma**refu.
Vazi **hili** ni zuri - **Ma**vazi **haya** ni **ma**zuri.
Rinda **hili** ni fupi - **Ma**rinda **haya** ni **ma**fupi.

## Mama afua nguo



# Alama za hesabu

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| a li pa za<br>**alipaza** | mbu zi<br>**mbuzi** | ma pa cha<br>**mapacha** |
| wa li o sa li a<br>**waliosalia** | m si tu<br>**msitu** | O jwa ng'<br>**Ojwang'** |

Tarakimu

| | | |
|---|---|---|
| 10 - **kumi** | 20 - **ishirini** | 30 - **thelathini** |
| 50 - **hamsini** | 80 - **themanini** | 100 - **mia moja** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li po kuwa<br>**walipokuwa** | wa me beba<br>**wamebeba** |
| ku wa rudisha<br>**kuwarudisha** | a li wa peleka<br>**aliwapeleka** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Huyu** | | **Yule** |
|---|---|---|
| Mbuzi **huyu** anakimbia | - | Mbuzi **yule** anakimbia. |
| Ndege **huyu** anapendeza | - | Ndege **yule** anapendeza. |
| Fisi **huyu** ni mlafi | - | Fisi **yule** ni mlafi. |
| Ng'ombe **huyu** ametulia | - | Ng'ombe **yule** ametulia. |



## Mzee Ojwang'

Mzee Ojwang alikuwa na mbuzi kumi. Aliwapeleka malishoni karibu na msitu mkubwa. Walipokuwa wakila nyasi, fisi akaja na kumla mmoja. Mzee Ojwang alipaza sauti na kuita, "Wooiii! Nisaidie. Fisi! Mbuzi wangu! Wooooiii! Fisi! Mbuzi wangu!" Wanakijiji wakaja haraka kumsaidia Mzee Ojwang. Wengi walijaribu kumfukuza fisi. Wengine wakapiga simu kwa idara ya ulinzi wa wanyama pori. Lakini fisi tayari alikuwa amerudi kwenye msitu mkubwa. Wanakijiji walimsaidia Mzee Ojwang kuwarudisha nyumbani mbuzi waliosalia. Kesho yake, Mzee Ojwang alijawa na furaha alipopata mbuzi wake wawili wamezaa mapacha.

# Alama za hesabu

Soma silabi na maneno.

ku o nge za

**kuongeza**

ku zi di sha

**kuzidisha**

ku to a

**kutoa**

ku fa u lu

**kufaulu**

ku ga wa nya

**kugawanya**

ku sa wa zi sha

**kusawazisha**

Soma sehemu za neno na neno lote.

wa na vyo dhani

**wanavyodhani**

hu ku elekeza

**hukuelekeza**

ku vi elewa

**kuvielewa**

ya na yo husisha

**yanayohusisha**

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
| --- | --- | --- |
| Alama **ya** hesabu | - | Alama **za** hesabu. |
| Alama **ya** kuongeza | - | Alama **za** kuongeza. |
| Alama **ya** kutoa | - | Alama **za** kutoa. |
| Alama **ya** kuzidisha | - | Alama **za** kuzidisha. |
| Alama **ya** kujumlisha | - | Alama **za** kujumlisha. |



## Alama za hesabu

Wanafunzi wengi hudhani kuwa somo la hesabu ni gumu. Ukweli ni kwamba somo hili sio gumu kama wanavyodhani. Kuna vitu kadhaa ambavyo ukivijua na kuvielewa basi hesabu huwa rahisi sana. La kwanza ni kujua alama za hesabu kama vile: alama ya kuongeza (+), alama ya kutoa (-), alama ya kugawanya (÷), alama ya kuzidisha (×) na alama ya  kusawazisha (=). Alama hizi hukuelekeza kutatua matatizo mbalimbali yanayohusu hesabu. Somo la hesabu hukupa ujuzi wa kuweza kufanya kazi mbalimbali. Kwa hivyo tunasoma hesabu ili kufaulu katika mitihani yetu na pia kwa ajili ya manufaa ya maisha ya baadaye. Ukitaka kufaulu ni lazima upende na kufanya bidii kwenye somo hili la hesabu.

# Alama za hesabu

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ku ga wa nya - kugawanya**


★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| nya | za | ku | di | ga | to |
| nge | zi | a | sha | o | wa |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| Umoja | | Wingi |
|---|---|---|
| **M**kuki huu ni mdogo | - | **Mi**kuki hii ni midogo. |
| **M**ti huu ni mkubwa | - | **Mi**ti hii ni mikubwa. |
| **M**situ huu ni mzuri | - | **Mi**situ hii ni mizuri. |
| **M**nazi huu ni mrefu | - | **Mi**nazi hii ni mirefu. |

## Mafumbo



Soma silabi na maneno.


| | | | |
|---|---|---|---|
| | ta ra ki mu | i shi ri ni | the la thi ni |
| | **tarakimu** | **ishirini** | **thelathini** |
| | i da di | ha m si ni | ti si ni |
| | **idadi** | **hamsini** | **tisini** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| ★ | wa na i penda | wana funzi |
| | **wanaipenda** | **wanafunzi** |
| | wa wili | wavu lana |
| | **wawili** | **wavulana** |

Sarufi: Soma maneno haya na tarakimu.

| Majina | | Tarakimu |
|---|---|---|
| Mia moja na hamsini | - | 150 |
| Mia mbili | - | 200 |
| Mia mbili na hamsini | - | 250 |
| Mia tatu | - | 300 |
| Mia tatu na hamsini | - | 350 |
| Mia nne | - | 400 |
| Mia tano | - | 500 |



## Tarakimu

Shule ya msingi ya Pomoni ina wanafunzi wengi. Jumla ya wanafunzi wa darasa la kwanza ni mia mbili. Idadi ya wasichana wa darasa la kwanza ni mia moja na wawili. Idadi ya wavulana ni tisini na wanane. Jumla ya wanafunzi wa darasa la pili ni mia nne na ishirini. Wasichana wa darasa la pili ni mia tatu na wavulana ni mia moja ishirini. Jumla ya wanafunzi wa darasa la tatu ni mia tatu hamsini na saba. Idadi ya wasichana wa darasa la tatu ni mia mbili na ishirini na ya wavulana ni mia moja thelathini na saba. Jumla ya wanafunzi wa shule ya Pomoni ni mia tisa sabini na saba.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ha ba ri | m mo ja | wa wi li |
| **habari** | **mmoja** | **wawili** |
| shu le ni | njo o ni | ra fi ki |
| **shuleni** | **njooni** | **rafiki** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| a li ye potea | tu m rudishe |
| **aliyepotea** | **tumrudishe** |
| tu ki m pata | tu wa rudishe |
| **tukimpata** | **tuwarudishe** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|
| Mtoto mmoja | 1 | Watoto wawili | 2 |
| Paka mmoja | 1 | Paka watano | 5 |
| Rafiki mmoja | 1 | Marafiki wanne | 4 |
| Mwalimu mmoja | 1 | Walimu watatu | 3 |
| Samaki mmoja | 1 | Samaki saba | 7 |
| Ndovu mmoja | 1 | Ndovu kumi | 10 |
| Msichana mmoja | 1 | Wasichana sita | 6 |
| Mwalimu mmoja | 1 | Walimu kumi | 10 |



## Wimbo wa kuhesabu

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Kuna mtoto mmoja aliyepotea na tukimpata tumrudishe shule.
Rafiki yangu njoo, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Watoto wawili waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule.
Rafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

Moja mbili tatu nne tano sita saba nane tisa habari ya shuleni. Watoto watatu waliopotea na tukiwapata tuwarudishe shule.
Rafiki zangu njooni, twende shuleni leo.

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ta no - tano**

★

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a | n | fu | ku | ba | e |
| ni | no | n | l | li | o |
| sa | ya | ne | tu | ti | mi |

Sarufi: Soma maneno na tarakimu.

●

| Majina | Tarakimu |
|---|---|
| Mia moja | 100 |
| Mia moja hamsini | 150 |
| Mia mbili | 200 |
| Mia mbili sabini | 270 |
| Mia tatu | 300 |

## Gazeti la baba



# Rangi za bendera

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| nye u pe | ki ja ni | nye ku ndu |
| **nyeupe** | **kijani** | **nyekundu** |
| nye u si | ki bi chi | dhi ha ka |
| **nyeusi** | **kibichi** | **dhihaka** |


Soma sehemu za neno na neno lote.

| | | |
|---|---|---|
| i me ni lea | tu li yo pigania | wa me ni sinya |
| **imenilea** | **tuliyopigania** | **wamenisinya** |
| twa ji vunia | tu si pendane | i ki pepea |
| **twajivunia** | **tusipendane** | **ikipepea** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| nchi **ya**ngu | - | nchi **ze**tu |
| bendera **ya**ngu | - | bendera **ze**tu |
| rangi **ya**ngu | - | rangi **ze**tu |
| | | |
| taifa **la**ngu | - | mataifa **ye**tu |
| gari **la**ngu | - | magari **ye**tu |
| koti **la**ngu | - | makoti **ye**tu |

# Rangi za bendera



## Rangi za bendera yetu

Nchi yangu imenilea, Taifa langu la Kenya,
Nchi yangu taitetea, wabaya wamenisinya,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

Rangi nne za bendera, ni muhimu nakwambia,
Nyeusi ya mwanadamu, uhuru kapigania,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia**.

Nyekundu ni ya damu, ilomwagika vitani,
Mashujaa kahitimu, mjini na vijijini,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia.**

Kijani rangi ya nchi, twaitetea hakika,
Tuipende hii nchi, sisi sote bila dhihaka,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia**

Rangi nyeupe ya amani, kwa nini tusipendane?
Kumpenda wako jirani, hakuna hata jingine,
**Bendera ikipepea, wakenya twajivunia**.

# Rangi za bendera

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| be nde ra | ma ri da di | nye ku ndu |
| **bendera** | **maridadi** | **nyekundu** |
| wa za le ndo | hu s ta wi sha | A f ri ka |
| **wazalendo** | **hustawisha** | **Afrika** |



Bendera ya Kenya



Bendera ya Tanzania



Bendera ya Uganda


Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| i na wakilisha | i li yo mwagika |
| **inawakilisha** | **iliyomwagika** |
| tu ki pigania | wa li o pigania |
| **tukipigania** | **waliopigania** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **-etu** | | **-enu** |
|---|---|---|
| Uhuru **wetu** | - | Uhuru **wenu** |
| Uchumi **wetu** | - | Uchumi **wenu** |
| Ushujaa **wetu** | - | Ushujaa **wenu** |

# Rangi za bendera



## Bendera yetu

Kila taifa ulimwenguni lina bendera yake ya kipekee. Taifa letu la Kenya lina bendera iliyo na rangi nne. Kila rangi ina maana yake. Rangi nyeusi inawakilisha rangi ya watu wa Kenya. Wengi wa wakenya, kama watu wengine barani Afrika, ni watu weusi. Rangi nyekundu inawakilisha ushujaa wa wazalendo waliopigania uhuru wetu. Pia inawakilisha damu iliyomwagika wakati wa kupigania uhuru wetu. Rangi ya kijani kibichi inawakilisha ukulima kwenye nchi yetu. Mimea huwa na rangi ya kijani kibichi. Rangi ya mwisho ni nyeupe. Rangi hii inawakilisha amani ya nchi yetu. Kwa kweli bendera yetu ni maridadi sana.

# Rangi za bendera

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **nye ku ndu - nyekundu**

★

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| the | ki | ni | ndu | ma |
| ji | nye | ku | si | lu |
| kaa | u | ja | pe | mbi |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

- Nyekundu kama damu.
Nyeusi kama makaa.
Nyeupe kama theluji.
Kijani kama nyasi mbichi.

## Wimbo wa taifa

**1**
Ee Mungu nguvu yetu,
Ilete baraka kwetu,
Haki iwe ngao na mlinzi,
Natukae na undugu,
Amani na uhuru,
Raha tupate na ustawi.

**2**
Amkeni ndugu zetu,
Tufanye sote bidii,
Nasi tujitoe kwa nguvu,
Nchi yetu ya Kenya,
Tunayoipenda,
Tuwe tayari kuilinda.

**3**
Natujenge taifa letu,
Ee ndio wajibu wetu,
Kenya istahili heshima,
Tuungane mikono,
Pamoja kazini,
Kila siku tuwe na shukrani.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| ku fu a ta | m shi ndo | ma zi ngi ra |
| **kufuata** | **mshindo** | **mazingira** |
| so ko ni | ma ga nda | shi mo ni |
| **sokoni** | **maganda** | **shimoni** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| wa li m fuata | wa li po fika |
| **walimfuata** | **walipofika** |
| ya li yo m fanya | a ka wa ambia |
| **yaliyomfanya** | **akawaambia** |

Sarufi: Soma sentensi hizi.

| **Umoja** | | **Wingi** |
|---|---|---|
| Ganda hili ni kubwa | - | **Ma**ganda haya ni **ma**kubwa. |
| Ganda hili ni dogo | - | **Ma**ganda haya ni **ma**dogo. |
| Ganda hili ni tamu | - | **Ma**ganda haya ni **ma**tamu. |



## Mazingira

Watoto wengi hupenda kufuata wazazi au walezi wao wanapoenda sokoni. Siku moja Diba na Habona walimfuata mama yao sokoni. Walipofika sokoni waliona watu wengi wakila ndizi na kutupa maganda njiani. Mara Diba na Habona wakasikia mshindo mkuu. Walipoangalia wakaona mama yao ameanguka chini. Wakamwambia, "Pole mama." Walipotazama zaidi wakaona ganda la ndizi lililokuwa limetupwa. Ni ganda hilo lililomfanya mama akateleza na kuanguka chini.

Hapo ndipo mama akawaambia wanawe kwamba ni muhimu watu watunze mazingira. Mbali na hatari ya kuanguka kwa sababu ya kutupa taka ovyo, mazingira pia huchafuka. Aliwaeleza kuwa takataka zote zinafaa kutupwa mahali panapofaa. Takataka zinafaa kutupwa kwenye pipa la taka au kwenye shimo, bali si barabarani.

Soma silabi na maneno.

| | | |
|---|---|---|
| da wa | m za zi | u go njwa |
| **dawa** | **mzazi** | **ugonjwa** |
| si nda no | da k ta ri | u nge dha ni |
| **sindano** | **daktari** | **ungedhani** |

Soma sehemu za neno na neno lote.

| | |
|---|---|
| zi na tu shinda | zi na tu linda |
| **zinatushinda** | **zinatulinda** |
| u ta hatarisha | u si sherehekee |
| **utahatarisha** | **usisherehekee** |

Sarufi: Soma maneno haya.

| **Maneno** | | **Kinyume** |
|---|---|---|
| dawa **tamu** | - | dawa **chungu** |
| dawa **nyingi** | - | dawa **chache** |
| dawa **kubwa** | - | dawa **ndogo** |
| dawa **mbaya** | - | dawa **nzuri** |
| dawa **ghali** | - | dawa **rahisi** |



## Dawa

Dawa za kila aina, naomba usichezee,
Ugonjwa wa kila namna, daktari muelezee,
Kuna chungu na tamu sana, mtoto sisherehekee,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Dawa za maji twapenda, ni tamu kama asali,
Za tembe zinatushinda, ungedhani ni pilipili,
Sindano zinatulinda, kutoka kwa homa kali,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Dawa usiweke ovyo, ni hatari kwa maisha,
Mtoto akila sivyo, uzima huenda kwisha,
Dawa ukiacha hivyo, maisha utahatarisha,
**Dawa usinywe dawa, bila mzazi kuwepo.**

Tumia silabi katika jedwali kuunda maneno.
Kwa mfano: **ma zi ngi ra - mazingira**

★

| | | | |
|---|---|---|---|
| ra | ma | wa | da |
| zi | si | za | nda |
| no | m | ngi | ga |

Sarufi: Soma maneno haya.

| Neno | | Kinyume | Neno | | Kinyume |
|---|---|---|---|---|---|
| ghali | — | rahisi | simama | — | keti |
| panda | — | shuka | lia | — | cheka |
| jenga | — | bomoa | juu | — | chini |

## Majumba ya Nairobi



# Kiswahili 2

## Kitabu cha Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Kiswahili kimetayarishwa na kuchapishwa chini ya mradi wa TUSOME. Kimeandikwa kufuatia mwongozo wa mawanda na mfuatano uliofanyiwa utafiti wa hali ya juu kwa miaka mitatu katika mradi wa kuboresha ujuzi wa hisabati na usomaji nchini. Utafiti huu uliegemea kubuni njia mwafaka za kufunza usomaji na ufahamu.

Vipengele muhimu na vya kipekee kuhusu hiki kitabu ni:

- Kitabu hiki kinafuata mtaala wa taifa la Kenya.
- Mazoezi ya somo yamefuata mpangilio wa mantiki kutokana na utafiti wa njia bora za kufunza Kiswahili katika darasa la kwanza na la pili.
- Kitabu hiki kina michoro ya kupendeza ambayo hufanya somo la Kiswahili liwe la kuvutia.
- Masomo katika kitabu hiki hujumuisha vijenzi vyote vya lugha ambavyo ni; kusikiza, kuongea, kusoma na kuandika.
- Mpangilio wa kitabu hiki umekusudia kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa uzoefu kwa sababu kinawapatia nafasi ya kukumbana na vijenzi vyote vya kusoma.

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

UKaid from the British people

**Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.**

**Januari 2016**